Hapa panachomoka uponyaji wa kweli wa utakatifu. Kama tutafanya kazi hivi na wale wengine, sio kwa saba-bu ya uoga au mali, lakini kwa sababu ya kitu kinachotusukuma kutoka ndani, basi, tunakiri kwamba, katika fum-bo la yule mwingine, kuna picha/mfano halisi wa Mungu.

THE TRUE IMAGE OF GOD IMPLIES THE RESPONSIBILITY OF AN INFINITE DYNAMISM.

The human being has a restless heart, be it to love, to investigate, for the politics, or for riches. The reason for this unrest is God: You have made us for you and our heart is restless until it finds rest in you. (St. Augustine, Confessions I, 1). The divine image can be not only a dynamism that attracts, but also a disturbance that scares. The effort of the human being to eliminate the restlessness in his heart has no reason, instead of supporting it until it find rest in God. The Christian does not feel perfectly installed in the finite world, but feels sent by God to “live in the finite world” although at the same time he confesses that it is not “his permanent home”.

THE IMAGE OF GOD IMPLIES A NEW METHOD OF APPROACHING GOD.

The whole creation aspires to God. The relationship is not adequately described by the infinite distance between Creator and creature, by the image of God in the human being, but has to have in account the relation impulse-goal. God let himself be known in the person as the goal of his impulse, but also as the power of this impulse. The human being transcends in himself. . But the projection of the person does not consists in getting outside of himself of what he already has in himself, but in searching outside of himself that which he has only vaguely in himself. God does not appear only as a distant being, but as a speaker in dialogue, who comes closer. By his “divine condition”, the humanity will have the boldness, that only Jesus has had: to call God Father. The things have sacramentality when they are seen “with the eyes of God”.

THE IMAGE OF GOD AS A PASSION OF THE HUMAN BEING.

To be a person is not a rest, but a journey and not a smooth walk, but a climbing. There is only one unique history. The image and likeness is not something that has been added to creation, but a way of being for the creature. What the Christians call “the su-

MFANO HALISI WA MUNGU HUMAANISHA WAJIBU WA MAENDELEO YASIYO KIKOMO

Binadamu anakuwa na moyo wenye kusumbuka, iwe katika mapenzi, udadisi, siasa au utajiri. Sababu ya kusumbuka huku ni Mungu: “Umetuumba kwa sababu yako na mioyo yetu haitulii mpaka ipate utulifu kwako” (Mt Augustino, Maungamo I, 1). Sura takatifu inaweza kuwa sio tu kitu kinachovutia lakini pia usumbufu wenye kuogofya. Juhudi za mwanadamu kuondoa usumbufu moyoni mwake hazina sababu, badala ya kuunga mkono hadi apate pumziko kwa Mungu. Mkristo hajihisi kama aliyewe kwa katika dunia yenye mipaka lakini huhisi kutumwa na Mungu “kuishi katika ulimwengu wenye mipaka” hata ingawa wakati uo huo huungama kuwa dunia ‘sio makao yake ya milele.’

MFANO/SURA YA MUNGU HUMANISHA NJIA MPYA YA KUMKARIBIA MUNGU

Maumbile yote humtamani Mungu. Uhusiano huu hauelezewi vya kutosha na nafasi kati ya muumba na kiumbe, kwa sura ya Mungu katika mwanadamu, lakini lazima kutia maanani uhusiano wa lengo la msukumo. Mungu alifanya mwanadamu amjue kama lengo la msukumo wake, na pia kama nguvu ya msukumo huo. Binadamu huenda zaidi ya utu wake binafsi. Mwelekeo wa mwanadamu hauhusu kupata kutoka nje kile kitu ambacho tayari ako nacho lakini kutafuta nje yake kile ambacho kimepunguka ndani yake. Mungu haonekani tu kama mzungumzaji ajaye karibu katika mjadala. Katika ‘hali yake takatifu’ binadamu atapata ujasiri ambao ni Yesu pekee alikuwa nao: ule wa kumwita Mungu Baba. Mambo hupata dhana ya usakramenti yanapotazamwa kwa “macho ya Mungu”.

MFANO WA MUNGU KAMA MAHABA YA MWANADAMU

Kwa mwanadamu sio pumziko lakini ni safari, tena matembezi magumu, kukwea. Kuna historia moja tu ya kipekee. Sura na mfano sio kitu kilichoongezwa katika uumbaji lakini kama njia ya kuweko kwa sababu ya kiumbe. Kile wakristo huita ‘cha kiungu’

pernatural”, cannot consist in fleeing from the natural; it is a truth which is new, ultimate, over the human. Above the humanity. A community, that tried to seek the supernatural outside this history, in a claimed particular space, will not be any more a Christian community, but a “superstitious” community. The fact, that we are image of God, obliges us to engage in transforming and leading the history in order to be a reflection of our profound reality.

3. Grace and sin

In tens of centuries of history, the human being has been often capable of rising up again out of the ashes: not only from political and economical ashes, but also from the many human ashes individuals have risen, communities and historic eras. This reviving has been a being reborn to a new open combat. It is a reviving that shows that all hope were never lost, neither all doors have been closed.

No doubt that humanity needs to be radically renewed. It is the language of the “new man” of Paul. This renovation has a double task: the reconstruction and the empowering of humanity. It is the work that God is ready to do in the person and with the person.

The reality of grace makes the difference between Christianity and all the Humanists. While these believe that the human being is no sinner, but only with the potentiality to become perfect, the Christian believes that the human being is sinful, but, not withstanding, able to be perfect. The same Spirit of God has made the infertile womb of history fertile and has created a new humanity, the new Adam, Jesus Christ. The empowering and renewal of humanity is nothing less than an empowering towards the divine.

Those who transmitted that “only human can be God himself, revealed to persons that are in search of their humanity that only humans can only be fully human if they are gods. “I have said that they are gods...although they die as humans” (Psalm 81: 6).

hakiwezi kuepukana na ‘vitu vya kawaida’; ni ukweli mpya, wa mwisho, kuhusu wanadamu. Juu ya binadamu. Jamii ambayo inajaribu kumtafuta Mungu nje ya historia hii, katika mahali fulani, haiwezi tena kuwa jamii ya kikristo lakini jamii ya ‘mazingaom-bwe’/ushirikina’. Ukweli kwamba tu mfano wa Mungu, hututa-ka tuigeuze na kuilekeza historia ili iwe akisi ya uhalisia wetu.

3. Neema na dhambi

Katika makumi ya karne za historia, mwandamu amekuwa akiweza kuinuka kutoka kwenye majivu: sio tu majivu ya kisiasa na kiuchumi, lakini pia majivu mengine mengi ambayo watu binafsi wameinukia kwake, jamii na vipindi vya kihistoria. ‘Kufunuliwa’ huku kumekuwa kuzaliwa upya kwa kiumbe katika mkabala mpya ulio wazi. Ni ufunuo unaoonyesha kwamba matumaini yote hayakupotea au milango yote kufungwa.

Bila shaka binadamu anahitaji mageuzi mapya. Ni lugha ya ‘mtu mpya’ ya Paulo. Kufanywa upya huku kuna majukumu mawili sambamba: kujengwa upya na kupewa nguvu kwa binadamu. Ni kazi ambayo Mungu ako tayari kuifanya katika mwanadamu na pamoja na mtu yule mwingine.

Uhalisia wa neema huonyesha tofauti kati ya ukristo na watu wanaojishughulisha na (maswala ya) mwanadamu. Wakati watu hawa wanaamini kwamba binadamu sio mtenda dhambi, lakini tu mwenye uwezo wa kuwa mtakatifu wakristo huamini kwamba binadamu ni mwenye dhambi, lakini hata hivyo aweza kuwa mtakatifu. Roho yule yule wa Mungu ameondoa utasa kutoka kwa kizazi cha historia na ameumba binadamu wapya, adamu mpya, Yesu Kristo. Kuupa ubinadamu nguvu na kuumba upya sio kitu kilichopungua kutoa uwezo kuelekea Utakatifu. Wale walisema kwamba “ni binadamu tu awezaye kuwa Mungu mwenyewe”, waliwafunulia watafutao ubinadamu wao kwamba, ni wanadamu tu wawezao kuwa binadamu kamili kama wao wamekuwa miungu. “Nimesema kwamba wao ni

Grace cannot be assimilated as a thing, but as a personal presence. It is a *personal relationship between God and us*. The Spirit in us does not love only God but also the human beings. God wants to take possession of human being, not only so that we would love Him, but in order to love other persons by means of us.

This renovation of human quality in Christian language is called *grace*. On one side, grace has to do with free gift and with gratitude. But even, it is related to “*thankful*” and “*graceful*”. It is the favor of God that makes a person lovable. The “being person” according to God, has to do with gratefulness, with to attract (but to attract because one loves) and with being able to smile. And the three things are there because one knows that he/she is loved by God. The Christian language never speaks of having grace, but of being in grace (as one says: to be in form) because grace does not have to be conceived as a thing, but as a way a certain thing is. The project of brother/sister opens to us the plan of son/daughter. And the divine filiation becomes historically real in the plan of brother/sister.

Although its beginnings are simple, grace is inserted in the full human plan: the plan of filiation and fraternity. One has to take in consideration that the gift of grace is a process, a life, including a battle. And this one has to affirm at the level of personal history and as global history. Grace takes place in the midst of this being human, of this world and this history full of sin. The world is not divided in sin and grace, but in each person, each situation, there is at the same time grace that fights to be born in the sin and sin that battles to kill grace.

Universality of grace. God offers his grace always to all human beings, including those who are outside the church. In order to explain the effect of grace in a person or the victory over sin, Paul created the word “justification”. To justify equals “to make just”, therefore to make a person good. The Pauline jus-

miungu... hata ingawa hufa kama wanadamu...” (Zab 81: 6). Neema haiwezi kupokelewa ndani ya mtu kama kitu, bali kama uwepo na mtu binafsi. *Ni uhusiano wa kibinafsi kati yetu na Mungu*. Roho aliyeko ndani yetu hampendi Mungu tu bali pia wanadamu. Mungu anataka kuwamiliki wanadamu, sio tu ili tumpende, lakini ili awapende watu wengine kupitia kwetu.

Kuumbwa upya kwa hali ya binadamu katika lugha ya kikristo kunaitwa *neema*. Kwa upande mmoja, neema hushughulikia zawadi isiyo na malipo pamoja na shukrani. Lakini, hata uhusiano na ‘*shukrani*’ na ‘*neema*’. Kinachomfanya mtu apendeke ni wema wa Mungu. Kulingana na Mungu, ‘kiumbe mtu’ huhusu kuonyesha shukrani, pamoja na kuvutia (lakini kuvutia kwa sababu ya kupenda) na pamoja na kuweza kutabasamu. Mambo haya matatu yako kwa sababu mtu anajua kwamba Mungu anampenda. Lugha ya Kikristo haiongei juu ya kuwa na neema, bali kuwa katika neema (kama isemwavyo: kuwa sawa) kwa sababu neema haichukuliwi kama kitu, lakini kama namna kitu kilivyo. Mradi wa dada/kaka unatuelekeza kwa mpango wa mwana wa kiume/kike. Na hali takatifu ya kuwa mwana wa kiume/kike inakuwa halisi kihistoria katika mpango wa dada/kaka.

Hata ingawa vianzo vyake ni vya kawaida, neema inaingizwa katika mpango kamili wa binadamu: mpango wa wana wa kiume/kike na undugu. Zawadi ya neema yafaa kuchukuliwa kama utaratibu, maisha, na hata vita. Haya yafaa kuthibitika katika kiwango cha historia ya mtu binafsi na ile ya dunia nzima. Neema hujitokeza katika mwanadamu huyu, ulimwengu huu una historia iliyojaa dhambi. Ulimwengu haujagawa katika dhambi na neema, lakini katika kila mtu, kila hali, wakati uo huo, kuna neema ambayo hupigania kuzaliwa katika dhambi na dhambi ipiganayo ili kuua neema.

Ujumla wa Neema. Mungu daima huitoa neema yake kwa wanadamu wote hata kwa wale walioko nje ya kanisa. Ili kuelezea athari ya neema juu ya mtu au ushindi dhidi ya dhambi, Paulo alizua neno: “kufanywa mwadilifu”. Kufanya adilifu ni sawa na ‘kufanya kuwa haki’, kwa hivyo, kumboresha mtu. “Ufanyaji adil-

tification is the transformation of the person, from inhuman in good and therefore plainly human. “Justification” can be substituted with “human realization”, “rehabilitation”, “forgiveness”, “liberation”. Grace begins to transform the person “justifying him”. This justification is something historic, that, at the same time, is present and continues to develop.

Paul in the chapters 5-8 of the Letter to the Romans, develops the following steps:

- Chapter 5: he establishes the fact of justification of the person as a consequence of grace;
- Chapter 6 (and part of 7): he presents the work of grace in the person as a process of liberation from (liberation from sin, the law, the human antiquity);
- In the 2nd half of chapter 7 he reminds the historic character of this liberation and his contradictory experience: the person feels himself at the same time free and enslaved.
- Chapter 8 presents the transformation effected by grace as liberation in order to (for works of the Spirit of God, and therefore, sons/daughters of God). The Holy Spirit of God is the most human of the person.

Luther defended a “justification” as only external, that left the person as sinful as before. The Council of Trento defended “grace” that makes the human being really worthy before God. For Luther, the goodness of the person is not a reality at all, it is pure myth and consists only in that God does not pay attention to the sinfulness and sees only with kind eyes, but in a way that nothing changes to the person, except the possibility of continuing confiding in a God notwithstanding its own disaster. The grace is the Spirit of God present in our hearts. It gives us the means to love as God loves us. The importance of justification is not in the name one gives to the gift of God, but in how one responds to it.

Grace as liberation of oneself. Grace is really grace if, in the person, it becomes a liberation from him/herself. It means that

ifu” huu wa Paulo ni ubadilisho wa mtu, kutoka kwa hali isiyo ya kibinadamu katika wema na hivyo kuwa binadamu tu. “Kufanywa juwa mwadilifu” ni sawa na “kujitambua kwa mwanadamu”, “kustawishwa” “msamaha”, “ukombozi”. Neemahuanzakumbadili huku ikimfanya kuwa mwadilifu. Kufanywa adilifu huku ni jambo la kihistoria ambalo, wakati uo huo liko na linaendela kuimalika.

Paulo katika sura ya Tano hadi ya Nane (5-8) ya Barua kwa Warumi, anafanya hatua zifuatazo:

- Sura ya Tano: anaanzisha uhalisia wa kufanywa mtu mwadilifu kama matokeo ya neema.
- Katika sura ya sita (na sehemu ya sura ya saba): anaonyesha kazi ya neema ndani ya mtu kama utaratibu wa ukombozi (ukombozi kutoka kwa dhambi, sheria na makosa ya kibinadamu);
- Katika nusu ya pili ya sura ya saba, anakumbusha historia juu ya ukombozi na tajriba yake ikanganyishayo: mtu huhisi kama mtumwa;
- Sura ya nane huonyesha ubadilisho unaoletwa na neema kama ukombozi ili (kwa kazi ya Roho wa Mungu, binadamu wawe wana wa kiume/kike wa Mungu). Roho mtakatifu wa Mungu ndiye sehemu ya utu kabisa ya mwandamu.

Luther alitetea “kufanywa mwadilifu” kama swala la nje tu, ambalo lilimwacha mtu akiwa mwenye dhambi kama awali tu. Mtaguzo wa Trenti ulitetea “neema” ambayo humfanya mwanadamu kukubalika mbele ya Mungu. Kulingana na Luther, wema wa mtu si jambo la kihalisi hata kidogo, ni jambo lisilowezakana na lawezezana tu iwapo Mungu hatatilia maanani dhambi za watu na bada la yake awatazame kwa jicho la ukarimu na huruma. Lakini kwa njia ambayo haibadili kitu chochote kwa mwanadamu, ila tu kundelea kuyaweka mambo yake kwa Mungu bila kujali hatari zake. Neema ni Roho wa Mungu aliyeko mioyoni mwetu. Hutupatia njia za kumpenda jinsi ambavyo Mungu hutupenda. Umuhimu wa kufanyika mwadilifu hauko katika jina ambalo mtu hutoa kwa zawadi ya Mungu, lakini katika njia anayoipokea zawadi yenyewe.

Neema kama ukombozi wa mtu binafsi. Neema ni neema kweli, kama ikiwa ndani ya mtu. Inamkomboa kutokana na nafsi yake.

is a coming out from self-love, self-pleasing and self interested Paul describes the change of situation of the Christian with these words: "Grace submerges our old man in the death of Christ, grafts him onto it and is buries him with him, in order that our old self 'the sinful person' would die and would be servant of sin anymore" (Rom 6: 3-13). Grace also grafts us in the resurrection of Christ so that we may live our new humanity.

To submerge in, to graft onto, be buried with, are synonyms that try to express a situation, whose dynamism, can be described as an experience of dead and life. This double change of situation of the Christian implies also a change in his conscience. Grace as liberation for others: the new humanity. The nucleus of the New Testament can be put together as follows: we are redeemed in order to love our brothers/sisters: "Do not seek your own interest, but rather that of others" (Phil 2: 4).

Is an inversion of interests really possible? To love concrete persons is extremely difficult and practically impossible; precisely therefore, when we love, it is God himself (or His spirit, or His grace) who loves them in ourselves. The work of the Spirit in us consists in the implantation of the person in the divine filiation, in order to be brother/sister and in the implantation of the person in the liberty of himself in order to be impartial.

Grace as fraternal filiation. "Put on the new man created according to God" (Eph.4: 24). Fraternity is for us humans simply impossible. It is only possible as 'grace'. "Objective truth in the human life" a person is created in order to..." The most profound definition of a being is "communion". Sin makes it impossible for the person to assume this being. Grace remakes a person for the living together and empowers him/her for communion.

The journey to fraternity supposes a change of trend of 180 degrees in the human trajectory. It supposes to leave the trajectory of wanting-to-be-like-gods (Gen 3: 5) and to enter in the slow trajectory of self emptying, in order to present oneself as

Ina maana ya kujitoa katika ubinafsi, hali ya kujifurahisha kwa mtu binafsi, na kujishughulikia mwenyewe. Paulo anaelezea mabadiliko ya hali ya wakristo kwa maneno yafuatayo: “Maana, mnajua kwamba...” (Warom 6: 3-13). Neema pia hutuweka katika ufufuko wa Kristo ili tuweze kushiriki ubinadamu wetu mpya.

Kutosa ndani, ‘kupachika’ juu ya, kuzikwa pamoja na, ni visawe vi-navyojaribu kuelezea hali ambayo maendeleo yake, yaweza kuelezewa kama tajriba ya kifo na uzima. Mabadiliko haya mawili ya hali ya mkristo huonyesha mabadiliko katika dhamiri yake. Neema kama ukombozi kwa wengine: ubinadamu mpya. Kiini cha Agano Jipya chaweza kuwekwa pamoja kama ifuatavyo: Tumekombolewa ili tuwapende kaka/dada zetu “Pasiwe na mtu anayetafuta faida yake mwenyewe tu bali faida ya mwenzake” (Fil 2: 4).

Je, kugeuzwa kwa nia kwawezekana? Kuwapenda watu wengine kwa uhalisi ni jambo ngumu kabisa na haliwezekani; kusema kweli, tunapopenda wengine, ni Mungu mwenyewe (au Roho wake au neema yake) anayewapenda ndani yetu. Kazi yake Roho ndani yetu hujumuisha kumweka mtu ndani ya undugu wa kimungu, ili awe kaka/dada na katika kuwekwa kwa mtu katika uhuru wa nafsi yake ili asiwe na ubaguzi.

Neema kama undugu wa kaka/dada. “Vaeni mtu mpya aliyeumbwa kwa mfano wa Mungu” (Efe 4: 24). Undugu kwetu wanadamu ni mgumu. Unawezekana tu kama “neema”. “Ukweli halisi maishani mwa mwanadamu”. “mtu ameumbwa ili...”. Ufafanuzi mwafaka wa kiumbe ni “komunyo”. Dhambi humzuia kuwa kiumbe hiki (cha komunyo). Neema humuumba upya mtu kwa kuishi pamoja na kumpa uwezo wa komunyo.

Safari ya undugu hupendekeza mageuzi makubwa katika njia pinde ya mwanadamu. Inapendekeza kuacha njia pinde ya kuta kuwa-kama-miungu (Mwa 3: 5) na kuingia katika njia pinde ya kujisafisha, ili kujiwasilisha kama mmoja wa watoao huduma...

one of many...serving unto death (Phil 2: 7-8). This trajectory is superhuman: like this the humans can be like God himself. Fraternity has a price that very often includes a self-giving of one's own life: martyrdom. When one loves and is ready to give his life for his brothers/sisters, then it is when grace is over abundant that redeems not only the brothers/sisters, but also even the murderers.

SIN

Sin is defined as a rupture of the relationship with God, with the person, with oneself and with the world. To this communion the human being is called by his proper vocation (cf. Puebla, 322). Mysteriously and paradoxically, the human being can take free options, that can go against his/her vocation of communion. In that way the contradiction of his/her own being is going to be revealed. This personal contradiction is manifested in the particular contradictions, concrete, historic, that people establish in our world, a world "of rich people and every time richer at the cost of the poor who are every time much poor" (Puebla, 30). And marginalizing his neighbour, the person rejects the Lord; negating his brother, he negates God (Mt 25: 36-51). In the hands of a person is the capacity to offer fraternity or injustice, conditions for life or for death, salvation or condemnation. The human wills are structured in society as forces, mechanisms or kinds of oppression or liberation; but, at the same time, behind every unjust structure there is a will, personal or collective, responsible: there is a will of rejecting of God and of others. The answer of humanity to God is given in history: in it people offer life in the way of God or we reject it, we side with sin or we take it away. The historic concretization is no fatality or mere structural mechanism, but personal responsibility before God and humanity.

To eliminate this possibility of communion opens the door to a series of deformations, that are justification and rationalization of our behaviour and the evil that afflict the majorities. *Duality of our existence:* We establish compartments that only correspond

hadi kufa. (Fil 2: 7-8). Njia hii pinde iko juu ya mwanadamu: kwa namna hii, wanadamu waweza kuwa kama Mungu mwenyewe. Undugu una gharama yake ambayo mara nyingi huwa ni pamoja na kutoa maisha ya mtu binafsi: kuuawa kwa ajili ya Injili. Mtu apendapo na akiwa tayari kutoa maisha yake kwa ajili ya kaka\dada zake, basi, wakati neema imezidi hukomboa sio kaka/dada pekee, bali pia wauaji.

DHAMBBI

Dhambi inafafanuliwa kama kuvunjika kwa uhusiano na Mungu, na mtu, na nafsi yako na ulimwengu. Kwa komunyo hii, mwanadamu ameitwa kwa wito wake ulio sawa. (cf. Puebla, 322). Kwa njia ya fumbo na kweli-kinzani, mwanadamu aweza kufanya uamuzi huru ambao waweza kwenda kimyume na wito wake wa komunyo. Kwa njia hiyo, mkinzano wa nafsi yake utafunuliwa. Mkinzano huu unadhihirishwa katika mkinzano fulani, halisi, wa kihistoria, ambao watu wameanzisha katika ulimwengu wetu, ulimwengu wa watu matajiri na kila mara wanatajirika zaidi kwa kuwanyonya maskini ambao wanazidi kudidimia katika umaskini” (Puebla, 30). Kwa kumtenga jirani, mtu anamkataa Bwana; kumkana ndugu ni kumkana Mungu (Mat 25: 36-51). Mikononi mwa mtu kuna uwezo wa kutoa undugu au dhuluma, hali ziletazo uzima au mauti, ukombozi au kuhukumiwa. Nia za watu zimejengeka katika jamii kama misukumo, mbinu au aina za dhuluma au ukombozi; lakini wakati uo huo, katika kila dhuluma kuna nia, ya mtu binafsi au ya watu kwa jumla, uajibikaji: kuna nia ya kumkataa Mungu na watu wale wengine. Jawabu la mwanadamu kwa Mungu limetolewa katika historia: kwake, watu hutoa maisha kwa njia yake Mungu au kuyakataa, kuunga dhambi mkono au kuyatoa maisha. Udhambi wa kihistoria sio jambo hatari, au mbinu za kimuundo tu, lakini ni jukumu la mtu binafsi mbele ya Mungu na wanadamu.

Kuondoa uwezekano huu wa komunyo hufungua mlango kwa msururu wa uharibifu ambao ni ufanyaji adilifu, na kubadilisha tabia za watu wengi. *Njia mbili za kuishi kwetu:* huwa tunaanzisha vigezo ambavyo huafikiana na Mungu au nafsi

to God or our individual “I”, without counting with others. They are compartments, that correspond only to the Spirit without being incarnated in the concrete life. They correspond only to an interior conversion, that does has no repercussion in the structures, a reform of exterior conditions, that does not see the heart.

From the contradictions and the ruptures, that he is producing around him, the human being can arrive at a confrontation of the truth of his human condition: not only does he break the relationship with others, but he is internally broken in his being. Not only does he create contradictions, but he is a mysterious contradiction: vocation to communion and broken communion, just person and sinner. And he has to learn to be a person in history, in this tension between grace and sin. He has to become conscious that his actions are going to bring life or death to others, but must let himself too be brought much more by the love that has called him.

The seriousness of sin:

“Where sin is plentiful, there grace is still more plentiful” (Rom 5: 20). Sin is to fail to true love for God and for others. It hurts human nature and it is against human solidarity. Sin is an offense to God: “Against you, against you only have I sinned, the bad things in your eyes I committed” (Ps 51: 6). As the first sin, it is disobedience, a rebellion against God for trying to be “like god”, pretending to know and determine good and bad (Gen 3: 5).

The roots of sin are in the heart of the person. To choose deliberately, that means, knowing it and wanting it, a grave thing against the divine law and, to the final goal of the person, it is to commit *a mortal sin*. This destroys in us the love without which eternal bliss is impossible.

Venial sin is a moral disorder that can be repaired by the charity that this sin takes away in us.

The repetition of sins, including venial ones, engenders vices and under these are the *capital sins*.

(This part has been taken from the Catechism of the Catholic)

zetu “mimi” bila kuwajali wengine. Wao ni vigezo vinavyoafikiana tu na roho bila kumwilishwa katika maisha dhabiti. Huafikiana tu na mageuzi ya ndani ambayo hayana athari katika miundo, mabadiliko ya hali za nje, ambayo haioni moyo.

Kutokana na ukinzani na utengano huu, ambao binadamu anajisababishia, binadamu anaweza kufikia katika ukinzani wa hali halisi ya kibinadamu: havunji tu uhusiano wake na watu wale wengine, lakini amevunjika ndani katika utu wake; hasababishi ukinzani tu, bali yeye mwenyewe ni ukinzani wa kifumbo: wito kwa komunyo na komunyo iliyovunjika, mtu wa haki na mwenye dhambi. Na ni lazima ajifunze kuwa mtu katika historia, katika mvutano huu kati ya neema na dhambi. Lazima afahamu ya kwamba matendo yake yataleta uzima au mauti kwa watu wale wengine, lakini ni lazima ajiruhusu kuvutwa zaidi na upendo ambao umemwita.

Uhalisia wa dhambi: “Sheria ilitokea, ikasababisha kuongezeka kwa uhalifu; lakini pale dhambi ilipoongezeka, neema iliongezeka zaidi” (Rom. 5: 20). Dhambi ni kukosa kuwa na upendo wa kweli kwa Mungu na kwa watu wale wengine. Hudhuru maumbile ya mtu na ni kinyume cha umoja wa wanadamu. Dhambi ni kosa kwa Mungu: “Wewe wataka unyofu wa ndani; hivyo nifundishe hekima moyoni” (Zab 51: 6). Kwa dhambi ya kwanza, ni kutotii, kuasi Mungu kwa kujaribu kuwa kama “Mungu”, kujifanya kujua na kutathmini mema na mabaya (Mwa 3: 5).

Shina la dhambi liko moyoni mwa mwanadamu. Kuchagua kimakusudi, hii humaanisha kwa kujua na kwa kutaka, jambo baya na kinyume cha sheria takatifu na kwa mujibu wa hatima ya mwanadamu ni kufanya *dhambi ya mauti*. Hii huharibu ndani yetu upendo ambao tukiukosa, pumziko la milele haliwezi kuafikiwa. *Dhambi ndogo* ni kosa ambalo laweza kusahihishwa kwa wema ambao dhambi hii huondoa kutoka ndani yetu.

Kuendelea kuanguka dhambini hata kama ni dhambi ndogo, huleta uovu na hivyo dhambi kubwa.

4. Conscience, passions and virtues

*(This part has been taken from the
Catechism of the Catholic Church)*

CONSCIENCE

The person, image of God, constructs himself actively by means of his power of self decision; and in that way, conscience is not limited to be a simple mechanical application of principles to the risks in life; *it is a to invent every time the way a person responds to the quality of the image of God*, fulfilling himself in truth.

“In the deepest part of his conscience a person discovers a law, that he has not given to himself, but that he has to obey, whose voice resounds, when it is necessary, in the ears of his heart, calling him always to love and to do good and to avoid evil...A person has, in his heart, a law written by God...Conscience is the most secret nucleus, the most sacred in a person, in which the person is alone with God, whose voice resounds in the most personal part of himself” (GS 16).

Present in the heart of a person, the moral conscience (cf. Rom 2: 14-16) orders him, in the opportune moment, to practice the good and shun the bad. It also judges concrete options, approving the good ones and denouncing the bad ones (cf. Rom 1: 32). It affirms the authority of the truth with reference to the supreme Good, to which the person feels attraction and whose commandments he embraces. The prudent person, when he listens to his moral conscience, can hear God who speaks to him/her.

The moral conscience is a judgment of reasoning, in which the human person recognizes the moral quality of a concrete act, that he thinks of doing, is doing or has done. The person is obliged to follow faithfully, in all that he says and does, what he knows that it is just and correct. By means of the saying of his conscience, a person perceives and recognizes the prescriptions of the divine law.

Conscience makes it possible to assume the responsibility of done acts. If we commit the bad, the just judgment of the conscience

4. Dhamiri, hisia na maadili.

DHAMIRI

Mtu, mfano wa Mungu, hujijenga kwa bidii kwa njia ya uwezo wake wa uamuzi wa kibinafsi; kwa njia hii, dhamiri sio tu mbinu ya kutekeleza misimamo katika hatari za maisha; ni kuvumbua kila wakati njia ambayo mwanadamu *huafikiana na thamani ya mfano wa Mungu*, huku akijitilimisha katika ukweli.

“Ndani kabisa ya dhamiri yake, mtu hugundua sheria ambayo hakujiwekea mwenyewe, bali ambayo lazima aitii. Sauti yake yasikika moyoni mwake wakati unaotakiwa inayomwita kupenda au kutenda kilicho chema na kuepuka kibaya. Kwani mwanadamu anayo sheria moyoni mwake iliyoandikwa na Mungu. Dhamiri yake ndio kiini cha ndani sana na siri ya mwanadamu, ndipo patakatifu ambapo yupo peke yake pamoja na Mungu; ambapo sauti yake yasikika” (GS 16).

Dhamiri ya kimaadili ndani ya moyo wa mtu (cf. Rom 2: 14-16) humwamrisha katika wakati ufaao, kutenda mema na kuepuka mabaya. Huhakika njia tofauti tofauti dhabiti, huku ikipitisha zile bora na kukashifu zile nzuri (cf. Rom. 1: 32). Huthibitisha mamlaka ya ukweli kwa mujibu wa wema mkuu ambao humvutia mtu na ambao mtu hukumbatia amri zake. Mtu mwenye hekima anapoyasikiliza maadili yake ya kidhamiri, anaweza kumsikia Mungu azungumzaye naye.

Maadili ya kidhamiri ni uamuzi wa tafakari, ambao kwake mtu hutambua thamani ya maadili ya tendo halisi, ambalo anafikiria kulitenda, analotenda au alilotenda tayari. Mtu anawajibika ku fuata kwa uaminifu, kwa yote asemayo au atendayo, yale anayojua kuwa ya haki na sahihi. Kwa njia ya kusema juu ya dhamiri yake, mtu huhisi na kutambua maelekezo ya sheria takatifu.

Dhamiri huwezesha kuchukua wajibu kwa matendo yaliyotendwa. Ikiwa tutatenda uovu, hukumu ya haki ya dhamiri yaweza

can be in us the witness of universal truth of the good and, at the same time, that is the bad of his concrete election. Making patent the committed fault, reminds of the forgiveness that he/she has to appeal the good that has to be practiced still and the virtue that has to be cultivated, without stopping, with the grace of God. The education of the conscience is a task for the entire life. From the first years on, awakens in a child the knowledge and the practice of the interior law recognized by the moral conscience. A prudent education teaches virtue; preserves from fear, from egoism and pride, from unhealthy feelings of guilt.... The education of a conscience is a guarantee for freedom and brings forth peace in the heart.

In the formation of conscience, *the word of God is the light on our path*, that is necessary to be assimilated in faith and in prayer, and puts it in practice.

THE VIRTUES

The virtue is a habitual and firm disposition to do good.

The human virtues are stable dispositions of understanding and will, that regulate our actions, order our passions and guide our conduct, according to reason and faith. They can be classified under *four cardinal virtues*: prudence, justice, strength and moderation (abstinence).

The moral virtues grow through education, through deliberate acts and with persevering efforts. Grace purifies them and lifts them up.

The theological virtues make Christians live in relation with the Blessed Trinity. They have as origin, motive and objective, to know God by faith, trusting and loving Him for himself.

There are three theological virtues: faith, hope and love (cf. 1 Cor. 13: 13). They inform and liven all the moral virtues.

The seven gifts of the Holy Spirit given to Christians are: wisdom, understanding, council, strength, knowledge, devotion and fear of God.

kuwa ndani yetu shahidi wa ukweli-enevu wa wema na wakati uo huo, kwamba huo ni uovu wa chaguo lake. Kwa kuweka wazi kosa lililotendwa, hukumbusha juu ya msamaha ambao mtu aweza kuomba; wema ambao lazima utekelezwe pia na maadili ambayo ni lazima yapaliliwe, bila kikomo, kwa neema ya Mungu. Elimu ya dhamiri ni jukumu la maisha yote. Kuanzia miaka ya mwanzo na kuendelea, ujuzi na tekelezo la sheria ya kindani itambuliwayo na maadili ya kidhamiri huamshwa ndani ya mtoto. Elimu yenye hekima hufunza maadili; hulinda kutokana na uoga, kujipenda na majivuno, kutokana na hisia baya za kuwa na makosa... Elimu ya dhamiri ni hakikisho la uhuru; huleta amani ndani ya moyo.

Katika kukua kwa dhamiri, *neni la Mungu ni mwanga njiani mwetu*, ambao wafaa kupokelewa katika imani na katika maombi na kutekelezwa.

MAADILI

Uadilifu ni tabia na msimamo dhabiti wa kutenda wema.

Maadili ya bindamu ni misimamo dhabiti ya kufahamu na yenye nia, ambayo hutawala matendo yetu, kuelekeza hisia zetu, kuongoza mienendo yetu kulingana na fikra na imani. Maadili yaweza kupangwa katika *makundi manne makuu*: busara, haki, nguvu na kujizuia.

Maadili hukua kwa njia ya elimu, kupitia kwa matendo yaliyodhamiriwa na juhudi za kuhifadhi. Neema hutakasa maadili na kuyainua.

Maadili ya kithiolojia huwafanya wakristo kuishi katika uhusiano na Utatu mtakatifu. Dhima na lengo la maadili ni kusaidia kumjua Mungu kwa njia ya imani, kumwamini, kumpenda kwa sababu yake mwenyewe.

Kuna maadili ya aina tatu ya kitheolojia: imani, matumaini na upendo (cf. 1 Kor. 13: 13). Hufahamisha na kutia uhai maadili yote.

Karama saba za Roho Mtakatifu ni: hekima, shauri, nguvu, akili, ibada, elimu na uchaji Mungu.

THE PASSIONS

The human person reaches happiness by means of his deliberate actions: the passions and feelings, that he|she experiments, can prepare and contribute towards it.

The term “passions” mean what affects the person and his|her feelings. By means of his emotions, the person experiences good and bad. Eminent examples of passions are love and hate desire and fear, happiness, sadness and anger.

In the passions, they are impulses of sensibility, there is neither moral good nor bad. But, according to how they depend or don't on reason or will, there is in them moral good or bad.

Emotions and feelings can be assumed by the virtues or distorted by vices. The perfection of moral good consists in that the person is not only moved by his will, but also by his “heart”.

SYNTHESIS

- We are creatures (clay, limited, finite). We are body, beings in relation, beings in the world, free beings, social beings. This reality is in tension until it reaches the fulfillment: to be sons/daughters of God.
- This plan has appeared in its maximum splendor in Jesus Christ. In him, we all can reach the goal of plenitude, of happiness.
- “To the image of Himself He created them”(Gen 1: 27). John speaks of the realization of the image as a divinization of the person, and this divinization means his authentic human being. The image of God implies the dignity of the human person, the responsibility of an infinite dynamism and a new modality of access to God. The image of God as passion of the human being.
- The reality of sin and grace are Christian expressions in anthropology, to the understanding of the human being. The human being is a sinner. But, in spite of it, capable of being made perfect. Grace is a personal relation between God and us. This communion makes me son/daughter and brother/

HISIA

Mwanadamu huafikia furaha kwa njia ya matendo ya makusudi: hisia ambazo anapitia zaweza kutayarisha na kuchangia katika furaha hiyo.

Neno “hisia” lina maana kile kinachomwathiri mtu na hisi zake. Kwa njia ya hisia zake, mtu hupata tajriba ya mema na mabaya. Mifano mwafaka ya hisia ni upendo na chuki, tamaa na uoga, furaha, huzuni na hasira.

Katika hisia ambazo ni njia za kuelezea fikra, hakuna mema au mabaya ya kimaadili. Lakini kulingana na kutegemea kwake kwa fikra na nia, ndani ya hisia hizi kuna mabaya ya kimaadili.

Hisia na hisi zaweza kupatikana kwa maadili au kuharibiwa kwa uovu. Maadili mema hupatikana ikiwa tu, mtu atatawaliwa sio na nia yake tu, bali pia na moyo wake.

HITIMISHO.

1. Sisi ni viumbe (udongo, wasio na uwezo, wenye udhaifu). Tu mwili, viumbe katika uhusiano, ujumbe duniani, viumbe huru, viumbe wa kijamii. Ukweli huu uko katika mvutano hadi ufikiapo kutimilika kwake: kuwa wana wa Mungu.
2. Mpango huu unajitokeza katika ‘utukufu’ wake ndani ya Yesu Kristo. Ndani yake, sote twaweza kufikia lengo la fanaka na furaha.
3. “Kwa mfano wake mwenyewe aliwaumba” (Mwa 1: 27). Yohane anazungumzia juu ya kutambuliwa kwa mfano huu kama kufanywa mtakatifu kwa binadamu, na kutakaswa huku kuna maana ya ubinadamu wake halisi. Mfano/sura yake Mungu humaanisha hadhi ya mwanadamu, jukumu la maendeleo yasiyo mpaka na njia mpya na mwafaka ya kumfikia Mungu. Mfano wa Mungu kama husudu ya mwanadamu.
4. Uhalisia wa dhambi na neema ni njia za kujieleza za ukristo katika anthropolojia, katika ufahamu wa mwanadamu. Binadamu ni mwenye dhambi. Hata hivyo, aweza ku-

sister. Sin is the rupture of the communion with God, with the person, with myself and with the world. Christians are dead to sin and alive for God in Jesus Christ (Rom 6: 11).

- Conscience is like to invent each time a way, with which I respond to my quality of God's image. The constant walk in the following of Jesus is forming in myself habitual dispositions (virtues). My whole being, my will and my "heart" (passions) is to live in Christ Jesus. My life is Christ (Phil 1: 21).

ASSIGNMENT

1. Describe how one considers in the Nomadic culture, a person; what is the place this person occupies in the evaluation of time, money, and interests, etc.
2. Write down three attitudes, which manifest, what living in the Spirit of Jesus in the Northern Region of Kenya means (grace) and against the spirit of Jesus (sin).

fanyika mwenye haki. Neema ni uhusiano wa kibinafsi kati yetu na Mungu. Komunyo hii hunifanya niwe mwana wa kike/kiume na kaka/dada. Dhambi ni kuvunjika kwa komunyo na Mungu, na mtu, na mimi mwenyewe na pia na dunia. Wakristo wamekufa katika dhambi na kuwa hai kwa Mungu ndani ya Yesu Kristo (Warom 6: 11).

5. Dhamiri ni kama kuvumbua njia mpya kila mara ya kuafikiana na thamani yangu ya mfano wa Mungu. Matembezi ya kila mara ya kumfuata Yesu ni kuunda ndani yangu misimamo ya tabia (maadili). Nafsi yangu yote, nia na 'moyo' (hisia) ni kuishi ndani ya Kristo Yesu. Kwangu kuishi ni Kristo (Fil 1: 21).

ZOEZI

1. Elezea jinsi mtu huonekana au huchukuliwa katika desturi ya watu waishio maisha ya kuhamahama; ni nafsi gani ambayo mtu huyu huchukua katika tathmini ya wakati, pesa na matarajio mengineo. n.k.
2. Andika mitazamo mitatu ambayo huonyesha jinsi kuishi katika Roho wa Yesu Kaskazini mwa Kenya humaanisha (neema) na dhidi ya Roho wa Yesu (dhambi).

HUMAN SEXUALITY AND THE LAW OF LOVE

1. Identification and sexual maturity in the Nomadic People of the Northern Region.
2. Sexual dimension of the human person.
3. The sexual “salvation”
4. To love God and to love one’s neighbour: the Ten Commandments

1. Identification and sexual maturity in the Nomadic People of the Northern Region

Sexuality is an integral force of the whole person. It identifies us as males or females. It gives us the opportunity to realize our vocation: to be for the other, to love. It helps us to transcend ourselves and to live our life in communion with God. “What is sex, what does it mean to be male or female, what do we understand by love, what kind of interpersonal relations characterize us, what peculiarities has our God as applied to the Nomadic People of the Northern Region’s culture?” While sexuality in our country was an integral element in our life, now coming into contact with the culture of the new era from outside, it has been taken into serious confrontation. There are now so many ways of thinking, so many different ways of understanding love, sex, interpersonal relations, God..., that a lot of wisdom is required to keep us true to ourselves .

The solution is not in adopting rigid and undisputable norms but, given the speed of changes and with the variety of understandings of life, we must try and recreate ourselves constantly in a sincere dialogue with ourselves, with the various cultures and with the Spirit of Jesus. The communitarian reflection is also neces-

UJINSIA WA MWANADAMU NA AMRI YA UPENDO

1. Utambulisho na ukomavu wa kijinsia wa Jamii ya waha maji wa Kaskazini mwa Kenya.
2. Vipengele vya kijinsia vya mwanadamu.
3. “Ukombozi wa” kijinsia.
4. Kumpenda Mungu na jirani: Amri kumi za Mungu.

1. Utambulisho na ukomavu wa kijinsia wa Jamii ya wahamaji wa Kaskazini mwa Kenya.

Ujinsia/uana ni sehemu ya ukamilifu wa mtu. Hututambulisha kama wake au waume. Huturuhusu kuendeleza wito wetu: kuwepo kwa ajili ya wengine, kupenda. Hutuwezesha kujikiuka na kuishi maisha yetu kwa komunyo na Mungu. Uana ni nini? Ina maana gani kuwa mume au mke, tunaelewa nini kwa upendo, ni mahusiano gani kati yetu ambayo tuko nayo, Mungu wetu ana sifa gani... katika utamaduni wa jamii ya kaskazini mwa Kenya? Kama uana katika nchi yetu ungekuwa kipengele cha jamii, kukutana na desturi ya kizazi kipya cha chini mwa nchi huchukuliwa kwa makabiliano makali. Kuna njia nyingi za kufikiria, njia tofauti za kuelewa upendo, kuingiliana kimwili, mahusiano kati ya watu, Mungu... kwamba hekima nyingi inahitajika ili kubaki tukiwa waaminifu kwetu wenyewe.

Suluhisho sio kushikilia msimamo ule ule na maadili yasiyojadi-liwa lakini ni katika kasi ya mabadiliko na kuelewa maisha kwa njia nyingi, kufanyika upya katika mazungumzo ya dhati na nafsi zetu, na desturi zetu na pia na Roho wa Yesu. Uakisi wa ujamaa

sary to maintain the rhythm towards the dignity of the person.

Every year thousands of girls have an abortion. Adolescents that are pregnant and have abortions or even give birth generally suffer negative consequences of a psychological, economical, emotional, moral order or health problems. These are factors that contribute seriously to the formation of poor family structures.

The modern society, in which we live, is enormously sensual, with an excess of sexual activity that is commercialized. This reduces human sexuality to the physical intercourse and does not consider sexuality as an integral part of the human person.

Nomadic people strongly value the family. It is a cradle of care and support; it gives values and maintains traditions and culture. The family includes not only blood relatives, such as grandparents, uncles and cousins, but also godparents and special friends.

Morality takes care that the actions of people be saved by Christ, and as such it has to do with the integral force inherent to sexuality.

ABORTION AND HOMOSEXUALITY: SOME ACTUAL ASPECTS OF HUMAN SEXUALITY.

Abortion. By abortion we understand the expulsion of the fetus from the mother's uterus before it has reached a stage of completeness that allows it to survive outside the mother's womb. Abortion as expulsion of the fetus or interruption of pregnancy is the object of juridical reflection (laws), medical and moral issues.

There exist two kinds of abortion: the spontaneous and the provoked one. The spontaneous abortion happens through natural causes, without free human intervention.

There are four different types of provoked abortion:

- Therapeutic abortion: when the continuation of the pregnancy is a danger to the life of the pregnant woman.

ni muhimu ili kudumisha mwelekeo kwa hadhi ya mwanadamu. Kila mwaka maelfu ya wasichana hutoa mimba. Wasichana (na hata wakinamama) ambao wanatunga mimba na baadaye kuitoa au kujifungua mbila ya kuo hupatwa na madhara mbalimbali kama vile matatizo ya kisaikolojia, kuathirika kiuchumi na kihisia, kukiukwa kwa maadili na matatizo mengine ya afya. Haya ni mambo ambayo huchangia sana katika miundo dhaifu ya kifamilia.

Jamii ya kizazi kipya ambayo tunaishi kwake, imezidi katika utiriri. Shughuli za mapenzi zimefanywa kuwa shughuli za kibiashara. Mambo haya yameshusa uana wa mwanadamu kama jambo la viungo vya uzazi bila kuuchukulia kama sehemu ya mwanadamu.

Jamii ya wahamaji huthamini sana familia. Ni chemchemi ya huduma, msaada, hutoa maadili na kuendeleza desturi na tamaduni. Familia hapa haihusishi tu baba, mama na watoto, nyanya na babu, wajomba na wanaami, bali pia wazazi wasimamizi na marafiki wa kipekee.

Maadili hujali matendo ya mwanadamu kwamba yanaokolewa na Kristo, nilazimayahusikenamsukumowamaisha, ambayoni uana.

UAVYAJI (UTOAJI MIMBA) NA UBASHA: BAADHI YA VIPENGELE VYA UANA WA MWANADAMU

Utoaji Mimba: Utoaji mimba ni kule kutoa vijuzi kutoka kwa kizazi cha mama kabla kiumbe husika hajafikia umri wa kuishi nje ya tumbo la uzazi.

Utoaji mimba ni swala la kutafakariwa kisheria, kitabibu na kwa misingi ya kimaadili.

Kuna aina mbili za utoaji mimba: utoaji mimba wa dharura/ajali na aina ya pili ni utoaji mimba wa kushinikizwa: utoaji mimba wa dharura hutokea kwa njia ya kimaumbile bila ya ushirika wa mtu.

Kunazo aina nne za utoaji mimba wa kushinikizwa:

- Utoaji mimba kwa sababu za kiafya: utoaji mimba huu hutokea pale ambapo mimba huhatarisha maisha ya mama.

- **Eugenic abortion:** provoked when there is certainty that the new being will be born with abnormalities or congenital malformations.
- **Humanitarian abortion:** provoked or induced when the pregnancy is a result of a violent act, for example, rape.
- **Psychosocial abortion or provoked abortion:** when the pregnancy is unwanted for social or psychological reasons. This is the kind of abortion that is most frequent and used as a method of birth control.

The official doctrine of the Church on the moral implications of abortion is clear and concrete. It has its foundation in the doctrine of the Bible and Christian Tradition, and can be formulated in three points: 1) as all human beings, the baby in the maternal womb has the right to life based in God and not in the parents or the authority of any other person; 2) there is no person or human authority with a valid title, nor is there any medical, eugenic, social, or moral justification by which one can deliberately dispose of an innocent life; 3) only “indirect abortion” is justified.

“Since the first century the Church has affirmed the moral evil of every procured abortion. This teaching has not changed and remains unchangeable. Direct abortion, that is to say, abortion willed either as an end or as a means, is gravely contrary to the moral law” (CIC 2271). “God, the Lord of Life, has entrusted to humanity the sublime mission of conserving life, a mission that must be fulfilled in a dignified manner. Therefore, life has to be protected with the utmost care from the moment of conception; abortion as well as infanticide are horrible crimes” (GS 51, 3).

Homosexuality. The moral reflection on the homosexual condition of the human being has to have a positive finality: to search for adequate ways, which means “ethical” ways, for the human realization of the person in question. In this context the temptation must be overcome of either condemning

- Utoaji mimba kwa sababu za kimaumbile: hushinikizwa wakati inapodhihirika kwamba mtoto atakayezaliwa atakuwa na ulemavu au udhaifu mkubwa.
- Utoaji mimba kwa sababu za kibinadamu: hushinikizwa wakati mimba imetokana na kitendo cha kubakwa kwa nguvu.
- Utoaji mimba kwa sababu za kisaikolojia au utoaji mimba ulioshinikizwa: hutokea wakati mimba haileti matokeo yataki-kanayo kwa sababu za kijamii au kisaikolojia. Huu ndio utoaji mimba ambao hufanyika mara nyingi na hutumiwa kama njia ya kupanga uzazi.

Mafunzo ya kidini ya kanisa juu ya utoaji mimba ni wazi. Shina la mafunzo haya ni msimamo wa Biblia juu ya mwanadamu na utamaduni wa kikristo na huweza kuorodheshwa kwa hoja tatu: 1) Maisha yote ya mwanadamu yakiwemo yale ya mtoto aliyeko tumboni, yana haki, katika msingi wa Mungu, kuishi na sio uamuzi wa mzazi au mtu mwingine yeyote yule; 2) Hakuna mwanadamu au mamlakayoyote ya mwanadamu yenye haki halisi, au maelekezoya kitibabu, kijamii au kimaadili, kuua mwanadamu asiye na hatia; 3) Ni “utoaji mimba usio wa moja kwa moja” ambao unakubaliwa...

“Tangu karne ya kwanza, kanisa limesisitiza uovu wa kila utoaji wa mimba. Mafunzo haya hayajabadilika na hayawezi kubadilika. Utoaji mimba wa moja kwa moja, hii ni kusema, utoaji mimba uliodhamiriwa kwa sababu moja au nyingine, ni kinyume kabisa na sheria ya maadili” (CIC 2271).

Mungu, Bwana wa maisha, amemwaminia mwanadamu jukumu la kuhifadhi maisha, jukumu ambalo lazima litekelezwe kwa namna yenye hadhi. Kwa hivyo, maisha lazima yalindwe kwa uangalifu mkubwa kuanzia upachikwaji mimba; utoaji mimba na mauaji ya watoto wachanga ni hatia kubwa za kutia hofu” (GS 51, 3).

Ubasha: Tafakari ya hali ya ubasha ya mwanadamu lazima iwe na mwisho mwafaka: utafiti wa njia mwafaka, yaani, njia za kimaadili, za kujitambua kibinadamu kwa mtu anayehusika. Maadili katika mada hii yatakwepa masaibu ya kuka-

We can explain it with an example of the guitar: there are different types of guitar: guitar for a solo, guitar for accompaniment, guitar for basso. The three instruments are guitars (the charisma of “presiding in the Lord”, but in the musical complex, each one of them has its particular place, its particular tune and when they play together (Bishop, priest, deacon) is when you enjoy the full harmony.

The Pope does not have a higher rank in the sacrament. He is the bishop of Rome, elected to succeed Peter in the service of the unity of the universal Church.

SUMMARY

- Through baptism we enter into the mystery of God and that makes us live in fullness the reality of our being sons/daughters and brothers/sisters. From this experience, our life enters into

wale mitume kumi na wawili walikutana na waungaji mikono katika huduma hii, na kabla ya kufa, walitafuta warithi wao. Warithi hawa kwetu sasa ni maaskofu. Kwa hivyo, ukamilifu wa sakramenti ya hatua takatifu katika imani ya Kanisa Katoliki ni maaskofu. Kama vile mitume, waliokuwa na waungaji mikono, maaskofu pia wako nao: hawa ni makasisi na mashemanzi. Kwa njia hii, tunasema ya kwamba, hatua takatifu zinahusisha: Shemanzi: yeye hutangaza Injili ya Yesu Kristo na kutoa ushuhuda wa Yesu kwa matendo yake ya huruma.

Padre/kasisi: zaidi ya kufanya kazi kama ile ya shemanzi, husherehekea Ekaristi, hutoa sakramenti ya kitubio, na kuwapaka wagonjwa mafuta; huongoza jumuiya. Huunda sehemu ya “prebesteri” (jumla ya wachungaji wote): pamoja na makasisi wengine, hutekeleza huduma ya komunyo pamoja na askofu. Askofu: husimama kama mirthi wa mitume, hisimamia sehemu ya kundi la watu wa Mungu liitwalo jimbo (Diocesi), kwa msaada wa mapadre, akiunganika pamoja na wale maaskofu wengine, wao wanalisimamia Kanisa duniani kote. Kwa ukweli, Askofu, padre na shemasi ni kama kivuli (shade) ya rangi sawa “Charisma” (kipaji) sawa, “ya kuwa msimazi pamoja na Bwana”.

Tukitaka, kueleza tukitumia mfano tunasema: kuna aina tatu ya “guitars”. Kwa sauti ya kwanza (solo), kwa “kuzindikiza” (accompaniment) ama “guitar” kwa sauti ya “bass” (basso). Viombo (instruments) hivyi vitatu ni guitars (kipaji cha kuongoza katika Bwana) bali katika mchezo wa kuigiza wa muziki kila kimoja kili kuwa na nafasi yake kenye, sauti ya pekee, na kusikia mapatano ya kweli.

Papa (Baba matakatifu): hana daraja ya juu kisakramenti. Yeye ni askofu wa Roma, aliyechaguliwa kuchukua mahali pa Petro katika huduma ya umoja wa Kanisa la dunia yote.

HITIMISHO

1. Kupitia kwa ubatizo, tunaingia katika fumbo la Mungu na hii inatufanya tuishi katika ukamilifu wa uhalisia wa wana wa kiume/kike na ndugu/dada. Kutokana na tajriba hii, maisha

a dynamic of fidelity (following Jesus) that makes us more and more sons/daughters and brothers/sisters (metanoia). In this journey we make an experience of making decisions against our reality of sons/daughters and brothers/sisters, something contrary to the historic plan of God (sin). The Spirit of Jesus does not abandon us, but through reconciliation we can reach our final goal: the communion between the Father and ourselves. Our body and the entire creation participate in the plan of brotherhood. The Spirit of Jesus knows how to heal our infirmities in his project and transform them into elements of life.

- Jesus lives today in our society: he gives meaning to life:
 - o life is a call to happiness;
 - o he brings the highest expression of human love:
 - o happiness comes by giving oneself unto the extreme.
- To be made for the other and to live this dynamic is the highest realization. Marriage and Holy Orders are signs of Jesus who continues loving to the extreme and gives his life in service.

TASK

1. Genesis Chapter 2 tells us about the enchanting communion between God, man and nature. In Chapter 3, the sin of Adam and Eve is narrated. Reflect and describe in what the sin consisted and what the consequences were.
2. Suffering and death are part of our existence. Today's society does not teach us how to suffer and still less how to prepare for death. From the point of faith and Christian wisdom, what can we offer to this society?
3. What does marriage mean nowadays for the Church in Northern Province of Kenya? Present three aspects.
4. God is Father and forms his family: the brotherhood. The priest is "father", sign of God who builds his family: the Christian community. Describe some traits in the priest for our times and place.

yetu yanaingia katika uaminifu endelevu (kufuata Yesu) ambao unatufanya tuwe wana wa kiume/kike na ndugu/dada (metanoia) zaidi na zaidi. Katika safari hii, tunapata tajriba ya kufanya maamuzi dhidi ya uhalisia wetu wa wana wa kiume/kike na ndugu/dada na kinyume na mpango wa kihistoria wa Mungu (dhambi). Roho wa Yesu hatuachi peke yetu, lakini, hutusukuma katika maisha yetu (mapatano) ili tuafikie lengo letu la mwisho: komunyo kati yetu na Baba. Miili yetu na maumbile yote hushiriki katika mpango wa undugu. Roho wa Yesu anajua jinsi ya kuugeuza udhaifu wetu katika mradi wake na kuufanya kuwa vipengele vya maisha.

2. Yesu anaishi siku ya leo katika jamii yetu: anayapa maisha maana:

- Maisha ni wito wa kuingia katika furaha;
 - Anaonyesha kiwango cha juu cha upendo wa wanadamu;
 - Furaha hupatikana katika kujitolea binafsi hadi mwisho.
3. Kuumbwa kwa sababu ya yule mtu mwingine na kuishi katika hali hii ya maendeleo ni utambuzi wa hali ya juu zaidi. Ndoa na hatua Takatifu ni ishara za Yesu ambaye anaendelea kutupenda hadi mwisho na kuyatoa maisha yake katika huduma.

ZOEZI.

1. Sura ya pili ya kitabu cha mwanzo inatuelezea juu ya komunyo ya kuvutia kati ya Mungu Awa na maumbile.

Katikasurayatatu, dhambi ya Adamuna Awainasimuliwa. Tafakarina uelezekile kilichokuweka katika dhambi hiyo namatokeo yake.

2. Mateso na kifo ni sehemu ya maisha yetu. Siku hizi, jamii haitufunzi kuteseka na hata kututayarisha kwa mauti. Katika mtazamo wa imani na heki-ma ya kikristo, ni nini tunachoweza kuipa jamii hii?
3. Kuoja kuna maana gani siku hizi kwa kanisa la Eneo hili la kaskazini mwa Kenya? Elezea maswala matatu.
4. Munguni Babana anaundafamiliyake: undugu. Kasisini "Baba" ishara ya Mungu ajengaye familia yake: jumuiya ya Wakristo. Elezea baadhi ya sifa za kasisi kwa nyakati na mahali petu.

PART FIVE

PASTORAL ACTIVITIES OF THE CHRISTIAN COMMUNITY

Evangelization is the proclamation of the Gospel to the world that the Church carries out through what she says, does and is. How does Christian Community carry out the plan of the Father through its work and make it visible through its many services?

- Through its service to humankind (Diakonia) and its total self-giving, whatever the consequences, the Christian Community makes known Jesus who builds up the Reign of God.
- Through its way of living and building community (Koinonia) the community reveals how Jesus builds up the family of God and fosters a way of life that is based on dialogue and communion.
- Through its witness, missionary activities, catechesis, and preaching, (Martiria), the community proclaims and manifests Jesus who is bringing about a new humanity through his word and works.
- In its liturgy the community celebrates with Jesus the “wonders” of the Reign of God, which constantly tends to its total fulfilment.

Part Five develops these major themes in three chapters:

- XIII Koinonia: the “Life” of the community;
- XIV Religious experience and Liturgia: the Community “celebrates” the building up of God’s Reign;
- XV Martyria: The community gives witness to the new humankind, and Diakonia: Community at the service of the world.

SEHEMU YA TANO

KAZI ZA KICHUNGAJI ZA JUMUIYA YA KIKRISTO

Uenezaji wa Injili ni ile kazi ya kuitangaza Injili kwa ulimwengu, kazi ambayo Kanisa hutekeleza kupitia kwa yale lisemalo, litendalo na jinsi lilivyo. Jumuiya ya kikristu hutekeleza vipi mpango wa Baba kupitia kwa kazi yake na kuifanya ionekane kwa njia ya huduma zake nyingi?

- Kwa njia ya huduma yake kwa wanadamu (Diakonia), pamoja na kule kujitolea kwa dhati, bila kujali athari za kujitolea huko, jumuiya ya Wakristu inamfanya Yesu anayejenga Utawala wa Mungu ajulikane.
- Kwa njia hiyo kuweko kwake na kujenga jumuiya (Koinonia), jumuiya inafichua namna Yesu anavyojenga familia ya Mungu na kuendeleza njia ya maisha ambayo msingi wake ni mazungumzo na komunyo.
- Kwa njia ya ushuhuda wake, matendo ya umisionari, mafunzo ya katekisimu, (Martyria) jumuiya inatangaza na kumdhihirisha Yesu, ambaye katika maneno yake na matendo yake anayafanya upya maisha ya binadamu.
- Katika liturjia yake jumuiya inasherekea pamoja na Yesu “mambo ya ajabu” ya Ufalme wa Mungu, ambayo daima yanaelekea katika utimilivu.

Sehemu ya Tano inajenga maudhui makuu yafuatayo katika sura tatu:

- XIII Koinonia: “Maisha” ya jumuiya
- XIV Maarifa ya dini na Liturjia: Jumuiya “inasherehekea” ujenzi wa Utawala wa Mungu.
- XV Martyria: Jumuiya inatoa “ushuhuda” kwa wanadamu waliofanywa upya, na
Diakonia: Jumuiya “yauhudumia” ulimwengu.

KOINONÍA: THE COMMUNITY'S “LIFE”

1. The Pastoral action of the Christian community.
2. How the community embodies an evangelizing church
3. Stages of the evangelizing process.
4. Koinonia: The Community as a Sacrament of God's Plan to bring all things together in Christ.

1. The pastoral action of the christian community

WHAT IS THE MEANING OF “PASTORAL ACTION”?

The word ‘pastoral’, which we are now using to speak of the action of the Church, refers to the action of a “shepherd”. The concept and reality of shepherding is deeply rooted in the culture of Israel. Its nomadic origins, the frequent allusions to the period of wandering, and a history in which the people's migrations left a profound mark on its very being, resulted in the image of the ‘shepherd’ acquiring enormous relevance for understanding God and for understanding themselves as a people. The image of the “shepherd” helped them to explain their history from the perspective of the love shown them by God.

God's intervention to rescue the people from slavery in Egypt and to guide them through the desert is presented using the image of a flock of sheep (Ps. 78:52). By forming them as a people God made them God's personal possession, a reign of priests, a holy nation (Exodus 19: 56). God's care for his possession is expressed in pastoral imagery; constantly leading them, always protecting them, liberating them from their enemies, handing over the promised land to them and partitioning it among them are presented in this vein (Ps.78:53-55). Sometimes, this care is expressed in terms denoting tenderness: “He tends his flock like a shepherd,

KOINONIA: “MAISHA” YA JUMUIYA

1. Matendo ya kichungaji ya jumuiya ya Kikristu;
2. Kanisa laeneza Injili kwa njia ya maisha na matendo ya Jumuiya.
3. Hatua utangazaji Injili;
4. Koinonia: Jumuiya kama sakramenti ya mpango wa Mungu wa kuleta vitu vyote pamoja katika Kristu.

1. Matendo ya Kichungaji ya Jumuiya ya Kikristu

NI NINI MAANA YA “MATENDO YA KICHUNGAJI”?

Neno “uchungaji”, ambalo tunatumia sasa kuzungumzia kazi ya Kanisa, lina maana ya kazi ya “kuchunga”. Dhana na uhalisia wa uchungaji ni swala lililokita mizizi zaidi katika desturi ya Waisraeli. Asili ya uhamaji ya jamii hii, kutajwa mara kwa mara kwa swala la kuhama, na historia inayoonyesha namna uhamaji wao ulivyoacha alama kubwa katika maisha yao, ni mambo yaliyochangia sura ya “mchungaji” kupata maana kubwa zaidi katika kumwelewa Mungu na kujielewa wao wenyewe kama jamii. Taswira ya “mchungaji” iliwasaidia kuelezea historia yao kwa mtazamo wa mapenzi ambayo Mungu alionyesha kwao.

Tendo la Mungu la kuwakomboa Waisraeli kutoka utumwani Misri na kuwaongoza jangwani linawasilishwa kwa taswira ya kundi la kondoo (Zaburi 78: 52). Kwa kuwafanya kuwa taifa, Mungu aliwafanya kuwa milki yake, kundi la makuhani, taifa teule (Kutoka 19: 5-6). Hali ya Mungu ya kuchuga milki yake inaelezwa katika taswira ya kichungaji; kuwaongoza kila mara, ulinzi wa kila daki-ka, ukombozi kutoka kwa maadui, kuwakabidhi nchi ya agano na kuigawa miongoni mwao kunawasilishwa kwa njia hii (Zaburi 78: 53-55). Wakati mwingine, utunzaji huu unatatajwa kwa msamiati unaodhihirisha wororo: “Atalilisha kundi lake kama mchungaji,

gathers the lambs in his arms, carries them close to his heart and cares for those that have young” (Is 40:11).

The return from exile is seen as God gathering his scattered sheep together again and as leading them back again to the land of their ancestors (Is 49:126; Zach 10:810).

In the New Testament, Jesus interprets his life story and mission from within the religious and cultural world view of his people, using pastoral terminology to present his own ministry. He encounters a situation in which the people are like a flock without a shepherd (Mt 9: 36; Mk 6:34). Not only is Jesus proclaimed the Good Shepherd, the flock takes on a new dimension of universality. The sheep that are not within the Jewish sheepfold also belong to him and he will unite them with the flock that he leads, so that there will be just one flock and one shepherd (Jn 10:16). The Risen Jesus entrusts Peter with the task of pasturing his sheep and his lambs (Jn 21:15-17).

In the same way that we call the actions of Jesus pastoral, we call pastoral the service of his Church to continue the mission of Jesus in the world until he comes again. “As the Father sent me, I send you. Receive the Holy Spirit” (20: 21). In the same way, those who carry out the pastoral ministry of the church are called shepherds.

The church engages with different peoples at diverse times in history, and she keeps adapting to the evolving demands of evangelization. The apostles and their communities were totally free in offering appropriate responses and adapting the structures of the Church. The way of organizing the community, the ministries of the community, the ways of praying, and places... have been in response to the diverse needs of the ages and locations of the Church. The Church achieves her mission in dialogue with history, and with the ‘present times’ and cultures of the world. Languages, buildings, vestments, juridical structures, mental

atawakusanya wanakondoo mikononi mwake, atawabeba kifuani pake, na kondoo wanyonyeshao atawaongoza polepole” (Isa 40: 11).

Kurudi kwao kutoka uhamishoni kunaleta picha ya Mungu kuwakusanya tena kondoo wake waliotawanyika na kuwaongoza kurejea katika nchi ya babu zao (Isa 49: 1-26; Zek. 10: 8-10).

Katika Agano Jipya, Yesu anatafsiri hadithi ya maisha na huduma yake kuanzia kwa mtazamo wa kidini na wa kidesturi wa watu wake na anaonyesha kazi yake kupitia kwa msamiati wa kichungaji. Anakutana ana kwa ana na hali ambapo watu wanaonekana kama kondoo wasiokuwa na mchungaji (Mt 9: 36; Mk 6: 34). Pamoja na kutangazwa kwa Yesu kama mchungaji mwema, kondoo wa kundi lake wanapata taswira mpya ya ujumuisho mpana. Kondoo ambao wametoka nje ya kundi la kondoo la Kiyahudi ni wake pia na atawaingiza ndani ya kundi aliongozalo, ili kuwe na kundi moja tu na mchungaji mmoja (Yohane 10: 16). Yesu Mfufuka anamwaminia Petero kazi ya kuchunga kondoo wake na wanakondoo wake (Yohane 21: 15-17).

Kwa njia ile ile ambayo twayaita matendo ya Yesu kuwa shughuli za uchungaji, vivyo hivyo, tumeitaja kama uchungaji huduma ya Kanisa ya kuendeleza kazi ya Yesu ulimwenguni hadi atakapokuja tena “ Kama vile Baba alivyonituma mimi, nami nawatuma nyinyi” (Yohane 20: 21). Vivyo hivyo, wale wanaofanya kazi ya uchungaji ya Kanisa wameitwa wachungaji.

Kanisa linatangamana na watu tofauti tofauti katika nyakati tofauti za kihistoria na Kanisa huweza kuingiana na mahitaji yanayobadilika ya uenezaji wa Injili. Mitume na jamii zao walikuwa huru sana kuyakubali mabadiliko na kukubaliana na miundo ya Kanisa. Njia ya kuratibu jamii, huduma za kijumuiya, njia na mahali pa sala ... haya yote yanalingana na hali zinazobadilika za kipindi cha kihistoria cha kanisa na eneo Kanisa lipo. Kanisa linaafikia malengo yake kwa kuzingatia historia na mambo ya wakati huu pamoja na kuheshimu tamaduni za watu. Lugha, mijengo, mavazi, taratibu za sheria, fikra na falsafa... hutiliwa

constructs, philosophical systems.... are recruited by the Gospel to be put at the service of evangelization. This is the only way for the Church to incarnate into a cultural context. Even though this dialogue may be costly and a source of problems, it is absolutely indispensable for the Church to continue to accomplish its mission.

CRITERIA FOR PASTORAL ACTION

Criteria that arise from continuing the mission of Christ.

- “Theandrical” action. This word means that since Jesus is both divine and human, divine and human actions are part of pastoral activity. Emphasizing the action of God in the life of the Church has provoked pastoral passivity, that is, unplanned pastoral activity or expecting God to do it all. Stressing the human dimension has historically led to pastoral naturalism that sees the activity and institution of the church as a result of human initiative and human concerns. Only a pastoral action that learns how to bring together the human and the divine dimensions could be guaranteed to be authentic.
- Sacramental action. The word sacrament speaks of mystery and symbol. The reality of the sacrament includes two elements: one visible and the other invisible. Jesus, the sacrament of the Father, said: “The one who sees me, sees the Father”. Vatican II explains Church as a sacrament of intimate union with God and of the unity of the whole human race (LG 1). The pastoral structures or the institutional aspect of the community are not just something added on to a spiritualistic theological understanding of the church, but they are the required component that identifies ecclesial action. The visible element must be the best window to what is not seen. Just by looking at us everyone should be able to understand the message that the Father’s Plan is one of universal “brotherhood”.
- Conversion. Through the incarnation, Jesus himself becomes the most perfect revelation of God. The pastoral action of the Christian community is marked by its smallness, sin, and con-

maanani na Injili ili kusaidia katika huduma za uenezaji Injili. Hii ndiyo njia ya pekee ya Kanisa ya kuweza kujiingiza katika mukadha wa utamaduni wa watu. Hata ingawa mkondo huu waweza kuwa ghali, tena chanzo cha matatizo, hauwezi kamwe kutupiliwa mbali ikiwa Kanisa litaendelea kuafikia malengo yake.

UTARATIBU WA KAZI YA KICHUNGAJI

Utaratibu unaotokana na kuendeleza huduma ya Kristo

- Kazi Teandrica. Neno hili linamaanisha ya kwamba, kwa vile Yesu ni Mungu na binadamu kwa wakati ule ule, matendo ya Kimungu na Kibinadamu ni sehemu ya kazi ya kichungaji. Kusisitizwa kwa jukumu la Mungu katika maisha kumezua hali ya uvivu wa kichungaji, hii ina maana ya kuwepo na majukumu ya kichungaji yasiyopangwa au kutarajia Mungu atende kila kitu. Kusisitizwa kwa majukumu ya watu kumeonekana kihistoria kwamba kunachangia wanadamu kutia bidii katika kazi za kichungaji na kuifanya asasi ya Kanisa kuonekana kama jukumu na jitihada za wanadamu. Uchungaji unaoweza kusemekana kuwa wa kweli na wa kuaminika, ni ule tu, unaojumuisha Umungu na ubinadamu.
- Kazi ya Kisakramenti. Neno sakramenti linatuelekeza kwa fumbo na ishara. Uhalisia wa sakramenti umeundwa kwa vipengele viwili: kimoja kinachoonekana na kingine kisichooonekana. Yesu, sakramenti ya Baba alisema: “Anionaye mimi amemwona Baba”. Mtaguso wa pili wa Vatikano ulifafanua Kanisa kama sakramenti ya kushikamana na Mungu kabisa na umoja wa wanadamu wote (LG 1). Miundo ya kichungaji au vipengele vya taasisi za jamii sio vitu vinavyoongezwa juu ya namna theolojia inavyoichukulia Kanisa, lakini ni viungo vinavyohitajika na vinavyotambulisha kazi ya Kanisa. Kinachoonekana lazima kiwe kama kioo cha kusaidia kuona kisichooonekana. Watu watuonapo, lazima waelewe ujumbe wa Mradi wa Baba wa kuwa na undugu kwa wanadamu wote.
- Mageuzi. Kupitia kujifanya mtu (umwilisho), Yesu mwenyewe

tingency. Church is at the same time both saint and sinner. The criterion of authenticity is the extent of ongoing conversion in the church's pastoral action.

CRITERIA SPRINGING FROM OUR JOURNEY TOWARDS THE KINGDOM

- **Historicity.** Jesus took part in a history of salvation, in which God has been at work in and through historical human events. The fullness of time that Jesus inaugurated gives history an eschatological dimension, in the sense that fulfilment is already present but is not yet fully manifest. The Church as the people of God is basically on pilgrimage. This characterizes and authenticates all the Church's pastoral action: following the dynamic movement of history, she journeys toward her total fulfilment, fraternity.
- **Openness to the signs of the times.** The values of the Kingdom do not exist only within the visible boundaries of the Church, but transcend them. The Spirit has stirred up values in the midst of humankind and of the world, without the Church having any exclusive claim over them. In order to fulfil her mission, the Church must search for the signs of the times, and know the world in which she lives, with its hopes and aspirations. To scrutinize the signs of the times means to read reality in the light of faith, comparing reality to the Gospel in order to discover through this reality the deepest questions of humankind, the answers for which humanity is waiting.

God moves history towards its final goal. The Signs of the times are those actions that help us to discover the presence of God and his action in the events of history. The community needs a great capacity to listen and discern in order to effectively focus its pastoral action.

anapata kuwa ufunuo mwafaka wa Mungu. Kazi ya uchungaji ya Jumuiya ya Kikristo inaonyeshwa na udogo wake, dhambi na mahitaji. Kanisa linakuwa na sura mbili kwa wakati mmoja: “mtu mtakatifu” na “mtu mwenye dhambi”. Kigezo cha uhalisia wa Kanisa ni kiwango chake cha mageuzi katika kazi ya kichungaji.

UTARATIBU UTOKANAO NA SAFARI YETU YA KUUELEKEA UFALME (WA MUNGU)

- Historia: Yesu alishiriki katika historia ya ukombozi, ambayo kwayo, kihistoria, Mungu amekuwa akitekeleza kazi yake kwa njia ya matukio ya binadamu. Utimilivu wa wakati ambao Yesu anaanzisha unaipa historia mtazamo wa nyakati za mwisho kwa njia kwamba, utimilivu uko lakini haujadhihirishwa kabisa. Kimsingi, Kanisa kama watu wa Mungu bado liko katika kiwango cha uhujaji. Hii inaonyesha na kuthibitisha kazi zake zote za kichungaji za Kanisa: kwa kufuata mabadiliko ya historia, Kanisa liko katika safari ya kutimilishwa kwake, kutimilishwa kwa undugu.
- Uwazi kwa ishara za wakati: Amali za Ufalme haziko tu katika mipaka ione kanayo ya Kanisa lakini huenda hata nje ya mipaka hiyo. Roho amechochea amali hizi miongoni mwa wanadamu na katika dunia, na Kanisa haliwezi kudai kwamba ndilo pekee linalomiliki amali hizi. Ili Kanisa liweze kutimiza jukumu lake, ni muhimu kwamba litazame ishara za nyakati, na lifahamu ulimwengu wake, matumaini na matamania yake. Kuchunguza ishara za wakati kunamaanisha: Kuusoma ukweli katika mwanga wa kimani, kulinganisha uhalisia na Injili ili kwa njia ya uhalisia huu, Kanisa liweze kujua maswali mazito ya ubinadamu na majibu ambayo ulimwengu unasubiri.

Mungu anaiielekeza historia katika lengo lake la mwisho. Ishara za nyakati ni matendo ambayo hutusaidia kutambua uwepo wa Mungu na matendo yake katika matukio ya historia. Jamii inahitaji uwezo mkubwa wa kuchanganua mambo ili iweze kuangazia

- **Universality.** The universality of salvation is the inspires action and is its criterion. The mission of the Church breaks down the barriers of time and space, to transform herself in offering and achieving salvation for everybody. This requires that the Church have the ability to incarnate herself in every culture firmly believing that every historic moment can become a time of salvation.

CRITERIA RESULTING FROM THE PRESENCE AND MISSION OF THE CHURCH IN THE WORLD

- **Dialogue.** When we place the task of the Church in its historic perspective and when we carry on the mission of Christ as his co-workers, we understand the action of the community as dialogue. God has spoken to humankind in many ways, and God keeps on communicating. Our pastoral action is a sacrament of this dialogue between God and humankind at this time.
- **Incarnation.** Jesus incarnated himself; making himself one of us. In doing so, he has shown the way that the action of the Christian community must follow: she should also incarnate. If the Gospel is not incarnated, it will never be assimilated by the peoples or cultures that make up our society: youth, workers, elderly people, etc.
- **Mission.** We are called to live and to be Church for just one reason: to carry on the mission. This is why we were born and only in the mission of Christ will we find our total fulfilment and happiness. Our community has lost strength, because in many cases it has lost its sense of mission. Only by losing ourselves, giving ourselves to the extent of handing over our lives, can we truly live and fulfil ourselves.

PASTORAL ACTIVITY AS SYNONYMOUS WITH EVANGELIZATION

The definition of “evangelization” has undergone a significant evolution. There has been a shift from understanding evangeli-

kazi yake ya uchungaji.

- Ujumla mpana. Ujumla wa wokovu hutia shime kazi na utaratibu wake. Huduma ya Kanisa inakiuka mipaka ya wakati na mahali, ili kujigeuza katika kutoa na kuafikia wokovu kwa wote. Hii inalhitaji Kanisa kuwa na uwezo wa kujigeuza katika kila utamaduni huku likiamini kwa dhati kwamba, kila kipindi cha historia chaweza kuwa wakati wa wokovu.

VIGEZO VINAVYOTOKANA NA UWEPO WA HUDUMU YA KANISA KWA ULMWENGU

- Mazungumzo. Tunapoweka jukumu la Kanisa katika mukadha wa kihistoria na tunapoendeleza kazi ya Kristo kama watenda-kazi wenzake, tunaelewa kazi ya jamii kama mazungumzo. Mungu amezungumza na wanadamu kwa njia nyingi, na Mungu anaendelea kuwasiliana na watu. Kazi yetu ya kichungaji ni sakramenti ya mazungumzo haya kati ya Mungu na wanadamu katika wakati huu.
- Umwilisho. Yesu alipata mwili; akajifanya mmoja wetu. Kwa kufanya hivi, anaonyesha namna kazi ya jumuiya ya Wakristo inavyopaswa kuwa: Kanisa lapaswa kupata umwilisho. Kama Injili haitamwilishwa, basi haitaweza kukubalika miongoni mwa watu na desturi zinazounda jamii yetu: vijana, wafanyikazi, wazee n.k.
- Huduma. Tumeitwa kuwepo na kuwa Kanisa kwa sababu moja tu: kuendeleza kazi ya Mungu. Tulizaliwa kwa sababu hii na ni kwa huduma ya Kristo tu ambamo tutapata kuridhika kabisa na kupata furaha. Jamii yetu imepoteza nguvu kwa kuwa, kwa njia nyingi, imepoteza mwelekeo wake kwa kazi yake kwa huduma. Ni kwa kujitolea tu, kujipeana hadi kufikia kiwango cha kutoa uhai wetu ndipo tutaishi kweli na kujikamilisha kabisa.

KAZI YA KICHUNGAJI NI SAWA NA UENEZAJI WA INJILI

Maana ya maneno “Uenezaji wa Injili” imepitia mabadiliko makubwa. Pamekuwa na mabadiliko ambayo awali maneno

zation as making the first announcement of the Gospel through the ministry of the word to those people who did not know the Good News to evangelization understood as the overall life of the Church.

“Evangelization is the total process by which the Church, the people of God:

- announces the Gospel of the Kingdom of God to the world;
- gives witness to the new way of being and living which Christ inaugurates among humankind;
- educates in the faith all those who convert to Christ;
- celebrates through the sacraments the presence of Jesus Christ and the gift of the Holy Spirit within the community;
- Permeates and transforms the whole temporal order with its power “

Evangelization is the Church announcing the Gospel to the world through everything she says, does and is. The Church is born from the evangelizing action of Jesus; he sends her out to evangelize in his name; she begins by evangelizing herself; she is the depository of the Good News that must be announced; she sends out evangelizers.

Which is the Good News that Catholic Church offers to the society in which we live? To the nomadic groups of the Northern Region of Kenya, the numerous and diverse tribes, migrants and farmers, teachers, politicians, traders, believers of Islam, or Ayyana, the Catholic Church announces the Good News that the fullness of life is possible, that it is possible to be happy and live with dignity, and that the formation of a society that is a “family” is already underway.

CHALLENGES OF OUR TIMES FOR RELIGION AND THE CATHOLIC CHURCH

Since the time of Vatican II our world has undergone critical changes, and due to the new realities, a different model of evangelization is required. We face a global situation, a world where

‘uenezaji Injili’ yalieleweka kurejelea utangazaji Injili kwa mara ya kwanza kwa njia ya huduma ya Neno kwa watu ambao hawajasikia Habari Njema na sasa maneno “uenezaji Injili” yaeleweka kama ujumla wa maisha ya Kanisa.

“Uenezaji wa Injili ni hali kamilifu ambayo kwayo Kanisa, watu wa Mungu:

- Hutangaza Injili ya Ufalme wa Mungu ulimwenguni.
- Hutoa ushuhuda wa njia mpya ya maisha ambayo Kristo anaanzisha kwa wanadamu;
- Kuwaelimisha katika imani watu wote wanaomkubali Kristo.
- Kusherehekea kwa njia ya Sakramenti uwepo wa Yesu Kristo na kipaji cha Roho Mtakatifu katika juimuiya.
- Kupenya na kubadili utaratibu wote wa kidunia na nguvu zake.”

Uenezaji Injili ni utangazaji wa Injili unaofanywa na Kanisa duni-ani kwa kila jambo linalosema, kutenda na namna lilivyo. Kanisa limezaliwa kutokana na uinjilishaji wa Kristo; analituma Kanisa kueneza Injili kwa jina lake: linaanza kwa kujiinjilisha lenyewe/ kujihubiria; Kanisa ndilo linalobeba Habari Njema ambayo ni lazima itangazwe; linawatuma ulimwenguni waenezaji Injili.

Kanisa Katoliki linatoa Habari gani Njema kwa jamii yetu? Kwa makundi ya jamii za kuhamahama za Kaskazini mwa Kenya, makabila mbalimbali, wahamiaji na wakulima, walimu, wanasiasa, wanabiashara, waumini Waislamu au Ayyana, Kanisa Katoliki linatangaza Habari Njema kwamba utimilifu wa maisha unawezekana, kwamba yawezekana kufurahi na kuishi maisha yenye heshima na kwamba uundaji wa jamii ambayo ni “familia” uko njiani.

CHANGAMOTO ZA NYAKATI ZETU ZA KIDINI NA KANISA KATOLIKI

Tangu wakati wa Mtaguzo wa Pili wa Vatican ulimwengu wetu umepitia mabadiliko makubwa, na kwa sababu ya hali hizi mpya, panahitajika njia tofauti za uenezaji Injili. Tunakabiliwa na hali

injustice is evident. Arguing (obstinate and confrontational attitudes to the point of total intransigence) replaces dialogue and a nostalgic return to old ways appears in many aspects of social life.

- In a secularized society religion is “scorned”. Religion and the Christian faith that were considered a fundamental value of life for a long time, are seen today as devalued products, no longer very meaningful in the view of many people.

Religious awareness expresses itself in many different ways: civil religion that includes the rituals and myths of the socio-political entity; religion of the masses: money, the sacred capitalist market, the cult of consumerism; secular religiosity: music, sports, hedonism, the earth goddess, worship of the body; religious fundamentalist movements, fascination with the occult and exotic, the dark enigma of fate and fascination with Satanism; religious syncretism: New Age, oriental approaches. In this sense society has become more religious: diverse groups have taken advantage of this religious sentiment to manipulate people in economics, politics and religion.

In this situation, religion needs to be re-examined, purified and deepened.

- In a pluralistic society religion is one option among many. The Christian faith seems to be a product like others, in competition with many other alternative proposals. Pluralism makes many people feel confused and perplexed, since all that the culture offers seems to enjoy the same level of credibility.
- Given the crisis that institutions and churches are undergoing, “official religion” does not seem very credible. Institutionalized religion is perceived as a product with a poor image and even worse management. Its messages are not very believable and are discredited.
- In post-modern culture, religion is an “ephemeral” experience. Our religion is in danger of becoming a disposable product in a society that is dominated in many dimensions by fragmenta-

ya kidunia, dunia ambayo imejaa ukosefu wa haki. Majibizano (hali mng'ang'ano na makabiliano hadi kiwango cha kushikilia misimamo mikali) huondoa mazungumzo na kurejesha watu katika njia za zamani kwa namna nyingi za maisha ya kijamii.

- Katika ulimwengu unaofuata mambo ya kidunia, Kanisa “linadharauliwa”. Dini na imani ya Kikristo mambo ambayo kwa muda mrefu yalichukuliwa kama maswala ya kimsingi ya maisha, leo yanadhalalishwa na hayana tena maana kubwa machoni mwa watu wengi.

Ufahamu wa kidini unajitokeza kwa njia nyingi tofauti: dini ya kiraia ambayo inahusisha ibada na imani za siasa za kijamii; dini ya umma: pesa, soko lililotakaswa la kibepari, tabia ya utumiaji mali; udini wa kidunia: nyimbo, michezo, anasa, mungu wa dunia, kuabudu mwili; makundi ya kimageuzi ya kidini, kufuata ibada za kichawi na za kigeni, maswala tata ya hatima ya uabudu wa shetani; utata wa kidini: Kizazi kipya, mwelekeo wa mataifa ya mashariki. Kwa hali hii jamii imejikita zaidi katika dini: makundi mbalimbali yamechukua fursa hii kuwahadaa watu kiuchumi, kisiasa na kidini.

Katika hali hii, dini inapaswa kuangaliwa upya, itakaswe na kuimarishwa.

- Katika jamii yenye uhuru wa kufanya jambo lolote lile dini ni mojawapo ya mambo hayo. Imani ya Kikristo yaonekana kuwa zao moja kama yalivyo mambo mengine, na iko katika ushindani na maswala mengi mengine ambayo mtu aweza kuchagua. Uhuru wa kutenda namna mtu atakavyo huwafanya watu kuchanganyikiwa na kushangaa kwa kuwa vitu vyote ambavyo desturi hii hutoa huwa vya viwango sawa.
- Kutokana na migogoro inayokabili taasisi na Kanisa, “dini rasmi” haionekani kukubalika. Dini iliyotaasisiwa yaonekana kama zao lenye sura dhaifu na mbaya zaidi kiusimamizi. Habari zake haziaminiki na zimedhoofishwa.
- Katika desturi za wakati ujao, dini itakuwa jambo la kupita tu. Imani yetu ya kidini iko katika hatari ya kupuuziliwa na

tion and the crisis of strong values. In fact, commitments and convictions are very often weak, provisional, and fragmentary. People are afraid of making long term commitments to definitive truth and values.

- Due to the separation of faith and life, and of faith and culture, religion lacks meaning. Faith seems to be strange, distant, and very often in conflict with the demands and values of culture and life.
- In our society, dominated by the “mass media”, religion is also is a fluid and fragmentary reality – an entertainment. Christian faith is practically reduced to the role of an ineffective countercultural proposal, a product overwhelmed by powerful forces of socialization and initiation, compared to which the religious experience seems insignificant and totally lacking in importance. For many people religion has a bad image.

AN UNSATISFACTORY RESPONSE: “ADMINISTRATION” AS PASTORAL SERVICE

- A Predominance of devotional and sacramental practices. In this model of pastoral activity, the liturgy and sacraments are central. Administering sacraments (i.e., the Eucharist, baptisms, confessions), the cult of saints, feasts, and devotions are the activities that absorb most of the pastoral attention. The purpose of these activities is to foster the religious practice of believers and its ideal is to engage the largest possible number of “practitioners”. Little attention is paid to personalizing and interiorizing the faith, since the experience of God and an option of faith are taken for granted.
- Intra-ecclesia Pastoral. This presupposes the existence of “a people who are already Christian”, and in this mind-set evangelization makes sense only for non-Christian peoples. As a consequence, missionary activity “ad extra” is almost nonexistent locally; there is no catechumenal activity, while Church

kutupwa katika jamii ambayo inatawaliwa pakubwa na migawanyinko na migogoro ya misimamo mikali. Kusema kweli, kuweka ahadi na kuaminika yanakuwa mambo magumu na yaliyosambaratika. Watu wanahofia kutoa ahadi za kudumu kwa ukweli na maadili mema.

- Kutokana na kutenganishwa kwa imani na maisha, na kutenganishwa kwa imani na utamaduni, dini inakosa maana. Imani inaonekana kuwa jambo ng'eni, la mbali na mara nyingi linalopingana na mahitaji na maadili ya utamaduni na maisha.
- Katika jamii yetu inayotawaliwa na “vyombo vya habari”, dini inapoteza uhalisia wake na kuwa kama chombo cha burudani. Imani ya Kikristo imedhalalishwa hadi kukosa uwezo wa kuiongoza jamii, imani hii inazidiwa nguvu na mienendo ya kuingiliana kijamii na faida za maisha, na hii inaifanya dini kukosa athari na kupoteza umuhimu wake kabisa. Kwa watu wengi, dini imepata picha mbaya.

SWALA LISILORIDHISHA: “UTAWALA” KAMA YA HUDUMA YA KICHUNGAJI

- Kuendelea katika matendo ya ibada na sakramenti. Katika muundo huu wa kazi ya kichungaji, liturjia na sakramenti hupewa kipaumbele. Utoaji wa sakramenti (Ekaristi, ubatizo, toba), sala kwa mitume, sherehe na ibada ni mambo ambayo huchukua nafasi kubwa katika uchungaji. Haja ya matendo haya ni kuendeleza matendo ya kidini ya waumini na nia yake ni kuwahusisha nambari kubwa iwezekanavyo ya “washiriki”. Hali ya kubinafsisha imani hakutiliwi amaanani kwa kuwa kujuana na Mungu na kuwa na imani kunachukuliwa hivi hivi.
- Uchungaji wa ndani ya Kanisa. Hii inachukulia kuweko kwa “watu ambao tayari ni Wakristo”, na katika mtazamo huu uenezaji Injili unachukuliwa kuwa tu kwa wale wasiokuwa Wakristo. Kutokana na haya, huduma za kichungaji zinafifia kabisa nje ya Kanisa; kunakosekana huduma za kikatekumeni,

activity is focused on pastoral ministry “ad intra”, fostering the life and religious practice of the community that remains faithful. Initiatives to help “fallen away” Christians come back to practice of the faith are pretty common, for example, through parish missions. The main objective of spiritual retreats, “cursillos” and days of prayer is to move people to receive the sacraments. The presence and action of the church in the world is limited and conditioned by the emphasis on formal worship. Understanding the Church in this way, based on anthropological dualism and a spiritualistic concept of salvation, focuses its pastoral activity almost exclusively on the spiritual dimension of the person. To exert an important influence in the social and political dimensions of community life in order to help transform society is not considered the responsibility of Church.

- Clerical dominance and emphasis on the institutional. At the institutional level, clericalism is the main feature of this pastoral style. The clergy (i.e., bishops, priests) and religious communities control and carry out most of the activities of the institution; the clergy may permit some lay people to take part in practical activities, but always under the direction of the clergy. The crisis of vocations and lack of priests is considered a great threat to the development of pastoral activity. Moreover, church life is overburdened with a series of complicated obligations, laws and rules that absorb much of the attention and efforts of the people in charge. Institutional, juridical and even financial matters are predominate in parish activities, to the detriment of effective evangelization.
- Ecclesio-centrism: In this pastoral perspective, the Church sees herself as the core of society, the unique owner of truth and salvation, guardian of the values of the Kingdom, with which she practically identifies herself. Church thinks that she is fulfilling her mission by reaffirming herself and growing, gaining conquering the largest number of followers, and regaining means of exercising power and influence.

na wakati u huo kazi za Kanisa zinaangazia uchungaji wa ndani kwa ndani, huku kazi hiyo ikiendeleza maisha na matendo ya jamii ambayo bado inashikilia imani. Mikakati ya kujaribu kuwarejesha Kanisani waumini walioteleza ni nyingi sana kwa mfano kwa njia ya parokia. Madhumuni kuu kuwa na vipindi vya kutafakari na siku za maombi ni kujaribu kuwafanya watu kupokea sakramenti. Uwepo na utendaji wa Kanisa ulimwenguni umejifunga na kujikita katika kutilia mkazo kuabudu kwa njia iliyo rasmi. Kwa kulielewa Kanisa kwa njia hii, kwa msingi mpana wa kiantropolojia na dhana ya kiroho juu ya wokovu, kunafanya kazi ya kichungaji karibu iangazie tu kipengele cha kiroho cha mwanadamu. Swala la kuleta mabadiliko katika maswala ya kijamii na kisiasa maishani mwa watu ili kuiboresha jamii lachukuliwa kama sio jukumu la Kanisa.

- Kutamalaki kwa viongozi wa kidini na kutilia mkazo sana katika taasisi. Katika kiwango cha taasisi, viongozi na uongozi wa kidini ni maswala makuu ya utaratibu huu wa kichungaji. Viongozi wa kidini (i.e. maaskofu, makasisi) na jumuiya ya kidini huthibiti na kuendeleza shughuli nyingi za Kanisa; viongozi hawa wanaweza kuwaruhusu waumini wa kawaida kutekeleza majukumu Fulani lakini chini ya uangalizi wa viongozi hawa. Mgogoro wa miito na ukosefu wa makasisi ni tishio kubwa kwa maendeleo ya kazi ya uchungaji. Juu ya hayo, maisha ya Kanisa yanakabiliwa na mzigo mkubwa wa majukumu magumu, sheria na kanuni, mambo ambayo huchukua muda mrefu na nguvu za wasimamizi. Maswala ya kitaasisi, kisheria na hata ya kifedha ni mambo ambayo yamejaa katika shughuli za parokia na hulemaza uenezaji Injili.
- Kanisa kujichukulia kama kiini cha mambo: Katika mtazamo huu wa kichungaji, Kanisa linajichukulia kama kiini cha jamii, linaona kama ndilo lenye kumiliki ukweli na wokovu, ulinzi wa amana za Ufalme, na lajitambulisha kwa mambo haya. Kanisa hufikiria kwamba linatekeleza kazi yake kwa kujithibitisha na kuimarika, kujipatia wafuazi wengi na kujipatia njia za

This kind of pastoral ministry does not have any future. Our current situation, the new age that is just being born, presents a challenge to religion, to the Catholic Church. At the core of everything is the need to reform our identity as Church and as an experience of faith within a society that is undergoing a deep and dynamic transformation. We need to clarify the specific and incisive characteristics of our mission, both as individual persons and as a community. In preparing for the future, where are we going? And what is our role in shaping the history of humankind? The Church is living a time when it is simply necessary to walk with courage towards what is new and unexplored. It is necessary to choose a path that brings us to the experience of God in Jesus Christ and to opt for a Church that is herself a living Gospel and an evangelizer. It is necessary to have the courage to pass from a pastoral practice of administration (of sacraments, courses, catechism...) to the pastoral ministry of evangelizing.

2. How the community embodies an evangelizing church

EVANGELIZATION: A HISTORIC ABOUT-FACE AS THE CHURCH COMMITS TO TAKING UP THE CHALLENGE.

At every level of the Church's life it is necessary to strengthen its ministry of evangelizing so that once again ongoing personal conversion and maturing faith may constitute the true and effective criteria of belonging to the Church and taking part in its mission. Deciding to devote oneself to evangelization, "the grace and proper vocation of the Church" (EN 14) is a choice so loaded with critical consequences that we may speak about a historic turn around in the history of the Church.

To place oneself in a state of evangelization means taking up the challenges presented by secularization, disbelief and pluralism, as well as to make our best efforts to overcome the serious crisis

kutekeleza nguvu na mvuto wake.

Aina hii ya uchungaji haina matumaini ya kuendelea kuwepo siku za usoni. Hali yetu jipya, kizazi hiki ambacho chaendelea kuzaliwa kinaleta changamot kwa dini, kwa Kanisa Katoliki. Kwa vile Kanisa ni kiini cha kila kitu, pana haja kuimarisha utambulisho wetu kama Kanisa na kama wenye imani miongoni mwa jamii ambayo inapitia kipindi cha mageuzi mengi makubwa. Tunapaswa kufafanua hasa nia yetu na dhima ya huduma yetu, tukiwa mtu binafsi au kama jumuiya. Tunapojitayarisha kwa siku za usoni, tunaelekea wapi? Tena jukumu letu ni lipi katika kujenga historia ya mwanadamu? Kanisa linaishi wakati ambapo pana haja kutembea kwa ujasiri kuelekea mambo mapya na yale ambayo hayajafumbuliwa. Ni muhimu kuchagua njia itakayotupeleka kukutana na Mungu kwa njia ya Yesu Kristo na kuchagua Kanisa ambalo lenyewe ni Injili hai na lienezalo Injili. Ni muhimu kuwa na ukakamavu wa kupita hatua ya uchungaji unaojikita zaidi katika utoaji wa (sakramenti, kosi, mafunzo ya katekumeni...) hadi kwa uchungaji unaoeneza Injili.

2. Namna jamii inavyochukulia kanisa litangazalo injili

UTANGAZAJI: MTAZAMO WA KIHISTORIA KANISA LIJITOLEAPO KUCHUKUA JUKUMU HILI.

Katika ngazi zote za maisha ya Kanisa, ni muhimu kuimarisha huduma yake ya kueneza Injili ili tuirudie hali ya awali ambapo mageuzi ya mtu binafsi na kukomaa kiimani kunaweza kuwa kigezo muhimu na halisi cha kuwa muumini wa Kanisa na kushiriki katika huduma yake. Mtu kujitolea mwenyewe katika uenezaji Injili, “neema na wito mwafaka wa Kanisa” (EN 14) ni uamuzi ambao una matokeo ya kina ambacho tunaweza kuongea juu ya mabadiliko makuu katika historia ya Kanisa.

Kujiweka katika hali ya kueneza Injili inamaanisha kukabiliana na changamoto zinazoletwa na hali ya kufanya mambo kidunia, kutoamini na kufuata mikondo mingi, ikiwa ni pamoja na kufanya

of credibility that the Church is facing. A great effort to give witness and to be authentically Christian is required if we want the Good News of the Reign of God to be credible. This effort is required, not only in particular moments, or in some aspects of the Church's activities, but in the whole life and reality of Church. It isn't enough that Church form and prepare volunteers or specialists or have "agencies" for evangelization; rather, it pertains to every aspect of the Church's life and everything is put in question.

- Evangelization requires an effort to focus the whole Church on the essential, in order to rediscover her Christian identity in terms that are culturally meaningful today, so that through the whole body of her traditions, rites, creeds and religious practices, she can present a heart that beats with the pure and transformative Gospel message.
- Evangelization obliges the Church to rediscover herself and re-express her identity and mission, namely, to be in the world a "word" that reveals the newness of the Reign of God. This entails accepting a dynamic and radical process of renewal based on the Word of God and abandoning ourselves in complete poverty to have as our only strength the power of the Word. It would not make any sense to "evangelize" by organizing publicity campaigns, or making use of the propaganda tools and the power plays with which we are all too familiar.
- Evangelization should move the Church to go out from herself to be the "servant of humankind", and be totally devoted to carrying out her saving proclamation. It does not make any sense to conceive of evangelization as a kind of "emergency rescue operation", in order to hold onto or restore her status or to recover lost sources of influence and prestige. Nor does it make sense to re-launch proselytising propaganda in order to gain new followers and to multiply the number of members.

bidii ya kweli ili kukiuka migogoro inayokabili uaminifu wa Kanisa. Panahitajika juhudi kubwa ili kutoa ushuhuda na kuwa wakristo halisi ikiwa tunataka Habari Njema za Utawala wa Mungu kuaminika. Juhudi hizi zinahitajika, sio tu katika vipindi fulani maalum, au tu katika maswala fulani ya kazi za Kanisa bali katika maisha yote ya Kanisa na uhalisia wake. Haitoshi kwa Kanisa kuunda makundi ya watu wanaojitolea kueneza Injili au wataalamu au “wakala” wa uenezaji Injili; badala yake, jukumu hili linahusisha vipengele vyote vya maisha ya Kanisa na kila kitu ndani yake kinahusishwa.

- Uenezaji Injili unahitaji juhudi za kutazamisha Kanisa lote kwa mambo yaliyo muhimu, ili lijikumbushe utambulisho wake wa Kikristo kwa taratibu ambazo zina maana katika nyakati hizi, ili kwa njia ya tamaduni zake zote, ibada, imani na kazi za kidini, liweze kuwasilisha moyo unaodunda kwa ujumbe wa Injili halisi na yenye kuleta mabadiliko.
- Uenezaji Injili unatoa jukumu kwa Kanisa kujitambua upya na kuelezea upya utambulisho wake na huduma yake, hii ni kusema, kuwa ulimwenguni “neni” linalofunua upya wa Utawala wa Mungu. Hii inahusisha kukumbatia hali mpya kabisa ya kujiimarisha upya kwa msingi wa Neno la Mungu na kujitolea kabisa katika umaskini na kulichukua Neno kama chemchemi ya pekee ya nguvu yetu. Haitakuwa na maana yoyote kueneza Injili kwa njia ya mikutano ya umma au kwa kutumia vyombo vya propaganda miongoni mwa njia zingine ambazo tumezizoea sana.
- Uenezaji Injili unapaswa kulitoa Kanisa nje ya nafsi yake na kulifanya kuwa “mtumishi wa wanadamu”, na kujitolea kabisa kuendeleza utangazaji wake wa wokovu. Haina maana yoyote kuuchukulia uenezaji Injili kama “harakati za dharura za kunusuru”, ili kushikilia au kujaribu kurejesha hadhi yake au kurejesha tena uwezo wake wa kuvutia uliopotea na hadhi iliyopotea. Pia hakuna maana yoyote kuanzisha tena kampeni au propaganda za kuwanyakua waumini wapya toka kwa wengine ili eti kuongeza idadi ya wafuasi.

The outcome needs to be to get the whole Church involved in a deep renewal project that is able to transform the historic meaning of the Church's presence in the world. We want to highlight some trends and common requirements for today's Church:

- *The fundamental objective and task of the Church's pastoral action: within the world, for the world, and at the service of the Reign (overcoming a church-centred perspective).*

